# Nipashe

Jumamosi Januari 19, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII


ISSN 0856 • Na. 0579817

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Magonjwa 10 yalioua watu wengi zaidi mwaka 2018

UKURASA 3




UKURASA 13

# JPM amzungumzia mrithi mikoba yake

**ATIA** shaka kama atahimili changamoto anazopitia, ataja sababu kumtumbua kigogo wa TCRA...*Endelea ukurasa wa 2*



Rais Dk. John Pombe Magufuli, akipeana mikono na Askofu Mkuu wa Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship (FGBF), Zacharia Kakobe, katika hafla ya makabidhiano ya Mfumo wa Kudhibiti Mawasiliano ya Ndani na Nje ya Nchi (TTMS), iliyofanyika Makao Makuu ya TCRA, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

### MAFANIKIO MAKUBWA UPANDIKIZAJI WA FIGO

WAGONJWA 19 wamepatiwa huduma ya upandikizwaji wa figo kati ya Julai na Desemba, mwaka jana...

**UKURASA WA 3**

### WAKALIA MAWE KWA UKOSEFU MADAWATI

WANAFUNZI waliojiunga kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Jakaya Kikwete, iliyoko katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma, mkoani Songwe...

## Mamia wafurika kutoa maoni muswada wa vyama

UKURASA 3

# RC aingilia kati DED, DSO kupigana ofisini



UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA, AS VITA HAPATOSHI LEO UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# JMP amzungumzia mrithi nafasi yake

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli, amesema hana uhakika kama mrithi wake ataweza kuhimili changamoto anazozipitia katika kutatua kero mbalimbali zinazowakabili Watanzania.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na wananchi, muda mfupi baada ya kushuhudia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ikikabidhiwa Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu (TTMS) wenye lengo la kusimamia mawasiliano ya ndani na nje ya nchi.

Alisema serikali ina changamoto nyingi ambazo zinatakiwa kutatuliwa na kwamba serikali ya awamu ya tano anayoiongoza, kuna magumu anayopitia katika kutekeleza majukumu yake.

Magufuli alisema kuna changamoto ambazo kama hazitatatuliwa na serikali ya awamu ya tano hazitatatuliwa maishani na haamini kama rais atakeyemfuata atazimudu.

"Ninawaambia ukweli kama kuna changamoto zilizobaki tusipozitatua katika awamu hii, sina hakika kama kiongozi atakayekuja atazitatua kwa sababu katika kuzitatua nakutana na changamoto nyingi na magumu mengi. Ni mengi mno na huwezi kuyataja yote ila ni magumu mno," alisema.

Aliongeza kuwa katika kukabiliana na changamoto hizo, anahitaji nguvu za Mungu na si vinginevyo.

**CHANZO KUMTUMBUA KIGOGO**

Rais Magufuli jana alifunguka na kutaja sababu za kumtumbua aliyewahi kuwa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Dk. Ally Simba, kuwa ni kushindwa kudhibiti hujuma za kuzuia kutekelezwa kwa mfumo huo.

"Nilipoingia madarakani mwishoni mwa mwaka 2015, sikuridhishwa na utendaji wa TCRA, hivyo nikaamua kwa makusudi kutafuta mkataba wa mkandarasi wa ujenzi wa mfumo huu," alisema.

Alisema alitumia vyombo vya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi wake na alipata mkataba ule na baada ya hapo alitengua uteuzi wa Dk. Simba.

INAENDELEA UK 8



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akionyesha michoro ya majengo ya Hospitali ya Uhuru, inayotarajiwa kujengwa katika kijiji cha Maduma, wilayani Chamwino, wakati alipokagua eneo hilo, jana). **PICHA: OWM**

## Wagonjwa 19 wapandikizwa figo ndani ya miezi mitano

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAGONJWA 19 wamepatiwa huduma ya upandikizwaji wa figo kati ya Julai na Desemba, mwaka jana, imeelezwa.

Idadi hiyo inafikisha wagonjwa 28 waliopata huduma hiyo toka hospitali ilipoanza kutoa huduma za kupandikiza figo Novemba, 2017.

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa ya utendaji ya wizara mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, katika ukumbi wa Bunge wa Pius Msekwa, jijini hapa.

Ummy alisema kutokana na huduma hiyo, imeokoa Sh. bilioni 2.24 ambazo zingetumika kupeleka wagonjwa 28 nje ya nchi kwa ajili ya matibabu ya kupandikizwa figo.

"Gharama ya huduma hii katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ni kati ya Sh. milioni 20 mpaka 30 kwa mgonjwa mmoja wakati nje ya nchi gharama ni kati ya Sh. milioni 100 mpaka 120. Serikali imeokoa Sh. bilioni 2.24 ambazo zingetumika kwa ajili ya matibabu hayo nje ya nchi," alisema.

Pia alisema Hospitali ya Taifa Muhimbili iliona jumla ya wagonjwa 30,189, Idara ya Utengamano ilihudumia wagonjwa 22,379, huku Idara ya Dawa ilihudumia maombi ya dawa 519,216 na Kitengo cha Figo kilitoa huduma za kusafisha damu kwa mizunguko 13,248, huku wagonjwa mahututi 960 walihudumiwa katika vyumba vya uangalizi maalumu

INAENDELEA UK 8


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
**40470 DODOMA,**

**17 Januari, 2019**

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe **24/01/2019** kampuni ya **Raphael Logistics Limited** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es Salaam Port kuelekea Kinyerezi,** gari hilo lenye namba za usajili:

   **696 DNR / T 459 CBB**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 20.0 |
| Upana | - | mita | 4.3 |
| Kimo | - | mita | 5.3 |

3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaam Port hadi Kinyerezi kupitia Tabata,** gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215007402


# RC aingilia kati DED, DSO kupigana ofisini

**Na Mwandishi Wetu,** MWANGA

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, ameingilia kati sakata la Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Zefrin Lubuva, kudaiwa kupigana makonde na Ofisa Usalama wa Taifa wa Wilaya (DSO), Abdi Musa.

Mghwira aliiambia Nipashe jana kuwa ametuma timu ya maofisa mbalimbali kwenda kuwahoji maofisa hao ili kujua chanzo chake na hatua za kuchukua.

"Tukio hilo ni la kweli, nimeshateua timu ya maofisa kwenda huko kuwahoji na ninadhani watakuwa wamejifungia mahali wanaandika taarifa yao ili waniletee niipitie," alisema.

"Baada ya kuipitia nafikiri leo jioni (jana) kama watakuwa wameemaliza, mimi mwenyewe (RC Mghwira) nitakwenda huko kesho (leo) kuwasikiliza wote wawili, itoshe kusema hivyo," alisema.

Kuchapana makonde kwa maofisa hao kumetokea zikiwa zimepita siku 24 tangu Mawaziri Selemani Jafo (Ofisi ya Rais, tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - Tamisemi) na Kapteni (mstaafu) George Mkuchika wa pia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kupiga kambi mkoani Kilimanjaro kutafuta suluhu ya uhusiano wa kutia shaka baina ya watendaji wa hao Rais.

Viongozi hao wanadaiwa kupigana jana mchana ikiwa ni saa chache tangu Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Aaron Mbogho, adaiwe kutoa amri ya kuwekwa ndani Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo.

Habari zaidi zinaeleza kuwa kabla ya tukio hilo, asubuhi kulikuwa na kikao katika ukumbi wa halmashauri ambacho mkurugenzi alipaswa kuhudhuria lakini hakutokea, hivyo kutuma mwakilishi.

Inadaiwa kuwa uamuzi wake wa kutuma mwakilishi, hakumpendeza ofisa usalama huyo na kuamua kumfuata ofisini kwake.

Baada ya kufika, inaelezwa kulitokea kutoelewana na ndipo wakashikana mashati na kuanza

INAENDELEA UK 8



Spika wa Bunge Mhe. Job Ndugai (Mb), akizungumza na Balozi wa Qatar hapa nchini, Abdullah Jassim Al-Maadadi, ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Mamia wafurika kutoa maoni muswada wa vyama vya siasa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI mamia ya watu wakifurika mkoani Dodoma kwa ajili ya kutoa maoni kwa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa, vyama vyote vya siasa vilivyosajiliwa leo vitatoa maoni yao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mohamed Mchengerwa, alisema leo vyama vyote 16 vitafika mbele ya kamati na kutoa maoni yao.

"Kesho (leo) tutakuwa na vyama vya siasa ambavyo vitakuja mbele ya kamati na wale wadau ambao wangependa kutuandikia maoni yao, basi watuandikie kwa sababu sisi tunafanya kazi sana na maoni ya wadau," alisema.

Alisema vyama hivyo leo na kesho pamoja na baraza la vyama vya siasa vitatoa maoni yao kwa kamati.

Mchengerwa alisema pamoja na kamati yake kupewa jukumu la kushughulika na miswada miwili, wa vyama vya siasa na wa marekebisho ya sheria mbalimbali namba 4 kwa mwaka 2018, wadau wengi wamejikita kutoa maoni kwenye muswada mmoja.

"Sheria ya vyama vya siasa imeleta mambo mengi. Tuna marekebisho ya Sheria namba 4 ya mwaka 2018, sheria ya vyama vya siasa lakini michango mingi ambayo imeletwa na wadau ni kuhusu sheria ya vyama vya siasa," alisema.

Alisema katika kipindi chake cha pili cha uenyekiti wa kamati hiyo, hajawahi kuona wadau wengi wakitoa maoni kwenye muswada kama ilivyo kwenye muswada huo.

"Tulikuwa na miswada mingi yenye changamoto na maslahi kwa Taifa ikiwemo ya madini lakini sijawahi ona watu waliowengi kama kipindi hichi.

"Kwa siku ya jana (juzi) pekee tumesikiliza maoni ya zaidi ya watu 220 wakiwamo wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Chama cha Wanasheria Wanawake (Tawla) na taasisi nyingi na wakati huo muda ulikuwa umeisha lakini kulikuwa na watu wengine takribani 100 nje wakisubiri kuingia kutoa maoni yao," alisema.

Mchengerwa alisema kwa siku ya jana wanatarajia kuwa na wadau 300 na ratiba inaonyesha watamaliza kupokea maoni yao saa nne usiku katika Ukumbi wa Pius Msekwa bungeni.

"Tutatoa fursa ya kuwasikiliza na sisi kama kamati tunajipambanua kwamba tunapenda maoni ya wadau kwa kuwa yanatusaidia kutunga sheria," alisema.

**KIFUNGU CHA 5 NA 6 MOTO**

Mchengerwa alisema maoni mengi ya wadau yamejikita kwenye kifungu cha 5 na 6 cha muswada huo, ambavyo vinahusu ofisi ya msajili.

"Wengine wanadai ofisi ya msajili imepewa madaraka mengi makubwa, pia kuna kifungu kinataka vyama vya siasa kupata fedha kupitia serikalini. Wengine

INAENDELEA UK. 8

# Magonjwa 10 yaliyoongoza kuua Watanzania wengi 2018

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetaja magonjwa 10 yaliyochangia vifo kwa kiasi kikubwa kwa mwaka 2018, huku homa ya mapafu ikiongoza kwa mwaka wa pili mfululizo na shinikizo la damu likiingia kwa mara ya kwanza katika orodha hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri wa Wizara hiyo, Ummy Mwalimu, alisema katika orodha ya magonjwa hayo 10, shinikizo la damu limechangia kwa asilimi 1.9 kwa kuchangia vifo 382.

Akitoa tathmini ya hali ya huduma za afya nchini kwa mwaka 2018, Waziri Ummy alisema shinikizo la damu halikuwapo katika magonjwa yaliyoongoza kwa kuchangia vifo nchini kwa mwaka 2017. "Shinikizo la damu katika magonjwa ambayo yalichangia vifo nchini kwa kipindi cha mwaka 2017 halikuwepo lakini mwaka huu limeingia hivyo basi kuna kila sababu ya kufanya jitihada katika kuhakikisha kuna mkakati wa kupambana na magonjwa yasiyoambukiza," alisema.

Alisema takwimu zilizokusanywa kupitia mfumo wa DHIS2 zimeainisha kuwa mwaka 2018 kumetokea jumla ya vifo 20,087 ikilinganishwa na vifo 19,693 mwaka 2017.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka miwili 2017/2018 homa ya mapafu imeongoza kwa kusababisha vifo na kwa mwaka 2017 ilichangia kwa asilimia 18.2 ya vifo vyote na mwaka jana kwa asilimia 12.9 ya vifo vyote. "Mwaka 2018 ugonjwa usio wa kuambukiza (shinikizo la damu) umejitokeza katika magonjwa 10 yanayoongoza kwa kusababisha vifo ambapo umechangia kwa asilimia 1.9 ya vifo vyote," alisema.

Aliyataja magonjwa mengine kuwa ni pamoja na kukosa pumzi kwa watoto uliochangia vifo 1,269 sawa na asilimia 6.3.

Ugonjwa wa moyo uliochangia vifo 1,253 sawa na asilimia 6.2, kifo cha mtoto tumboni (Ngozi imechumbuka) vifo 766 sawa na asilimi 3.8, Malaria vifo 693 sawa na asilimia 3.4, Ukimwi vifo 605 sawa na asilimia tatu.

Alisema magonjwa mengine ni kifo cha mtoto tumboni (ngozi haijachubuka) ilichangia vifo 540 sawa na asilimia 2.7, magonjwa mengine vifo 538 sawa na asilimia 2.7 na maambukizi katika damu kwa watoto vifo 496 sawa na asilimia 2.5.

Aidha, Waziri huyo alisema mahudhurio ya wagonjwa kwa mwaka jana yalikuwa 42,411,276 katika vituo vya kutolea huduma za tiba nchini ikilinganishwa na 54,478,926 kwa mwaka 2017.

Alisema kati ya hao wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 41,052,012 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 1,359,264 na kwamba idadi hiyo inajumuisha wa mahudhurio ya kwanza na ya marudio. Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Muhammad Bakari, alisema kuwa magonjwa yasiyoambukizwa yanaweza kuwa kikwazo baadaye kama hakutachukuliwa hatua za haraka kuyadhibiti.

Alisema magonjwa hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na mtindo wa maisha kama ulaji wa vyakula usiozingatia lishe bora, uzito kupitiliza pamoja na kutofanya mazoezi.

Kwa mujibu wa Prof. Makari, magonjwa hayo yasipodhibitiwa yanaweza kuisababishia serikali gharama kubwa za kutibu watu katika siku za baadaye.

# Wakalia mawe kisa ukosefu madawati

**Na Ibrahim Yassin,** TUNDUMA

WANAFUNZI waliojiunga kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Jakaya Kikwete, iliyoko katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma, mkoani Songwe, wanakalia mawe darasani kutokana na uhaba wa madawati.

Mbali na changamoto hiyo, pia shule hiyo inakabiliwa na ukosefu wa vyumba tisa vya madarasa na vilivyopo ni vitatu wakati mahitaji ni vyumba 13 kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya wanafunzi 474.

Tumaini David, mkazi wa Tunduma alisema jana kuwa ni aibu kwa serikali wilayani hapa kwa kuwa badala ya kufanya maandalizi mapema walisubiri hadi wanafunzi waanze masomo ndipo waanze kuhangaika.

"Hivi inaingia akilini kweli? Serikali inafahamu wazi kuwa kila mwaka wanafunzi wanachaguliwa kujiunga kidato cha kwanza, lakini wao hawashughuliki wanafanya harakati hizi wakati tayari muda wa masomo umeanza, wamekosea sana," alilalamika Tumaini.

Gidion Siwale, mkazi wa Tunduma alisema tatizo la madawati na vyumba vya madarasa ni kubwa na kwamba wako tayari kushirikiana na serikali kutatua, sambamba na kuweka mikakati ya pamoja ya upanuzi wa shule kuhepuka usumbufu licha ya kuwa hawajaandaliwa mapema.

Alisema suala la elimu ni muhimu na ilipaswa waelezwe mapema kuhusu ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kuwa wao ndio wenye shule na wangeweza kufyatua matofali, kusomba mchanga na kujenga na kwamba serikali ingefanya kazi ya kupaua lakini hilo halikufanyika.

Mwalimu Anna Sanga ambaye ni mkuu wa shule hiyo, licha ya kukiri wanafunzi kukaa kwenye mawe kwa kukosa madawati, alisema shule hiyo ina vyumba vitatu vya madarasa wakati mahitaji ni vyumba 12 kwa ajili ya kumudu wanafunzi 474 wa kidato cha kwanza.

Alisema jitihada za makusudi zinahitajika kunusuru wanafunzi hao ili waweze kusoma kwa raha pasipo kubanana na kwamba kutokana na changamoto hizo,anauhakika kuwa suala hilo litafanyiwa ufumbuzi wa haraka.

Kastori Msigara, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, alisema ni kweli jambo hilo lipo na kwamba halmashauri kwa kushirikiana na wadau wanafanya jitihada za haraka kuhakikisha majengo na madawati yanapatikana zinafanyika.



. Baadhi ya wahitimu wa Shahada ya Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia, wakiwa katika Mahafali ya 21 ya Chuo cha Diplomasia, yaliyofanyika Chuoni hapo, Kurasini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Kigwangalla avunja bodi ya TTB

**Na Renatha Msungu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, amevunja Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), baada ya kushindwa kusimamia menejimenti.

Bodi hiyo iliagizwa na Waziri kusimamia utengenezaji wa studio kwa ajili ya kutangaza utalii pamoja na mabango ya utalii barabarani kazi ambayo amesema kuwa imewashinda.

Wakati akichukua uamuzi huo, Kigwangalla pia ameipa menejimenti ya TTB miezi mitatu kujirekebisha vinginevyo atawatumbua wote.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kigwangalla alisema TTB imeshindwa kutekeleza maagizo ndani ya mwaka mzima tangu aagize na kusababisha kutukanwa bungeni na baadhi ya wabunge. Pia alisema bodi hiyo imeshindwa hata kuchapisha magazeti ya utalii na akiwa ndani ya ndege wananchi wamekuwa wakilalamika kwa kuwa ndege hiyo inapandwa na watu wa aina mbalimbali.

"Kwa kweli TTB mnaniangusha sana mmekaa kupokea mishahara lakini hakuna kazi mnayofanya," alisema Kigwangalla. Alisema aipa menejimenti miezi mitatu kuhakikisha inajirekebisha, vinginevyo atareje tena kwa ajili ya kuivuruga na kuteua wachapakazi.

Kwa mujibu wa Kigwangalla, bodi ya wakurugenzi wa TTB imekuwa ikilegalega na kusababisha menejimenti kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi kutokana na kuacha kutekeleza maagizo hata ambayo walistahili kuyatekeleza.

"Kwa kweli sihitaji utani katika kazi kwa sababu mnanifanya nionekana sifanyi kazi," alisema Kigwangalla.

Alisema anataka kuweka watu ambao ni wanachapakazi ili kuendana na awamu ya sasa ambayo inawajibika zaidi kwa wananchi kuliko kwa maslahi binafsi au kikundi cha watu wachache.

Waziri huyo aliwataka kila mmoja ajitathmini kulingana na kazi yake na kuwataka wabadilike ili kuhakikisha sekta hiyo inafanya kazi vizuri na wananchi wanaridhika.

Naye Meneja Masoko wa TTB, Geofrey Meena, alisema mpaka sasa wako katika hatua za mwisho za kukamilisha baadhi ya maagizo ya Waziri na kumtaka awape hadi mwisho wa mwezi kila kitu kitakuwa kimekamilika.

# Naibu Waziri akerwa bajeti kiduchu ya ardhi halmashauri

**Na Mwandishi Wetu,** RUFIJI

NAIBU Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, ameelezea kukerwa na tabia ya wakurugenzi wa halmashauri nchini kwa kuzitengea fedha kidogo idara za ardhi, hivyo kuzifanya kushindwa kutekeleza majukumu ipasavyo.

Akizungumza na watumishi wa sekta ya ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji mkoa wa Pwani jana, Mabula alisema wakurugenzi wengi katika halmashauri wamekuwa wakiifanya idara ya ardhi kama mtoto yatima.

"Ukienda katika halmashauri nyingi idara ya ardhi imekuwa kama mtoto yatima na ofisi zake haziridhishi kabisa kulinganisha na zile ofisi za idara zingine kama vile afya na elimu" alisema.

Kwa mujibu wa Mabula, katika halmashauri nyingi alizotembelea, bajeti katika idara za ardhi haizidi Sh. milioni nne tofauti na fedha za mapato ya ndani ingawa wakati mwingine hazipatikani zote.

Alisema tatizo linaloonekana ni wakurugenzi kutofahamu kama idara hiyo ina fedha nyingi na kuweka wazi kuwa iwapo halmashauri zitaamua kuisimamia sekta hiyo kikamilifu, zitajikusanyia mapato mengi kulinganisha na sekta zingine.

Mabula alisema katika ukusanyaji mapato ya serikali nchini, sekta ya ardhi inaweza ikawa sekta ya pili au ya tatu kwa kuingiza mapato mengi ikiwa nyuma ya taasisi zinazokusanya mapato moja kwa moja kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Mashaka Abdallah, alimweleza Mabula kuwa idara yake inakabiliwa na ufinyu wa bajeti inayotengewa kwa ajili ya kutekeleza kazi za ardhi na vitendea kazi kama kompyuta, mashine za uchapaji na usafiri.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 halmashauri yake ilipangiwa kukusanya Sh. milioni 15 na hadi Desemba 31, mwaka jana ilishakusanya Sh. milioni 16.7 ikiwa ni sawa na asilimia 111.6.

Kutokana na maelezo hayo, Mabula alisema ukosefu wa vitendea kazi unawakatisha tamaa watendaji wa sekta hiyo lakini pia unachangia watendaji hao kutofanya kazi vizuri na wakati mwingine kuwalazimu kutumia fedha zao za mfukoni kufanikisha kazi walizopangiwa.

Kuhusu ukusanyaji mapato kupitia sekta ya ardhi, Mabula alisema halmashauri nyingi zimekuwa zikifanya makisio kidogo ya fedha za makusanyo huku zikiacha fedha nyingi kwa wadaiwa na kuwataka watendaji kuweka makadirio kulingana na uhalisia wa madeni wanayodai.

Alitolea mfano wa halmashauri ya wilaya ya Rufiji kuwa pamoja na kuwekewa kiwango cha kukusanya Sh. milioni 15, ilikusanya Sh. milioni 16.7 kujivunia kuvuka lengo lakini kumbukumbu zilizoko wizarani zinaonyesha halmashauri hiyo inadai zaidi ya Sh. bilioni moja.

# Majaliwa ataka kasi ujenzi ofisi za wizara

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amemwagiza mkandarasi anayesimamia ujenzi wa Ofisi mpya ya Wizara ya Fedha na Mipango kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kuhakikisha anaongeza rasilimali watu ili kazi hiyo ikamilike kwa wakati na ubora unaotakiwa.

Majaliwa, alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara kukagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi mbalimbali za wizara katika mji wa serikali, eneo la Ihumwa jijini hapa.

Alisema zimebaki siku 21 pekee kukamilisha ujenzi huo na lengo la serikali ni kuona kazi hiyo imekamilika ifikapo Januari 31, mwaka huu, na kuonyesha hofu iwapo kazi hiyo itakamilika kwa wakati kwa kuwa hakuridhishwa na nguvu kazi iliyopo.

"Ninapokuta watu wachache huku kukiwa na kazi zisizohitaji kusubiri siku mbili kama kazi ya kuweka bimu, natarajia kuona watu wangekuwa wanaendelea kufanya kazi hizo," alisema.

Waziri Mkuu alisema mawaziri kutembelea ujenzi unaoendelea na kuona ubora wa majengo ni jukumu lao na wana uwezo wa kuonyesha kuridhika au kutoridhika na kazi inayoendelea.

Aliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuhakikisha mazingira ya eneo la wizara linapandwa miti kulingana na ramani ya majengo ya muda na ya kudumu.

Alisema kama watumishi walipo ni wachache, mkandarasi aongeze vijana ili ujenzi ukamilike mapema kwa kuwa kuna mafundi wengi mkoani Dodoma na nje ya mkoa huo wanaotafuta kazi.

Naye Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, aliahidi kusimamia maagizo ya Waziri Mkuu na kuhakikisha jengo linakamilika kwa wakati kwa kuwa hadi sasa asilimia 95 ya vifaa vyote muhimu vya ujenzi vimenunuliwa.

Kuhusu kuongeza nguvu kazi, Dk. Kijaji, alisema wizara itahakikisha mkandarasi anaongeza nguvu kazi kwa haraka kutoka mtaani au Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili ifikapo Januari 31, wizara ikabidhiwe jengo rasmi.

Dk. Kijaji alieleza kuwa Wizara iko tayari kuhamia katika jengo hilo Februari Mosi, mwaka huu.

Naye Mhandisi kutoka NHC, Elisante Olomi, anayesimamia ujenzi wa ofisi za wizara hiyo, alisema ujenzi unaendelea vizuri na mpaka sasa umekamlika kwa asilimia 75, huku akiahidi kuongeza mafundi wa kutosha.

HABARI KITAIFA

# TRA yatangaza msako wakwepa kodi

**Na Steven William** MUHEZA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA ) kwa kushirikiana na serikali ya wilaya ya Muheza, imetangaza msako mkali kwa wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi ya serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo, alitangaza kampeni hiyo jana wakati akizungumza na wafanyabishara wa wilayani hapa katika semina iliyoandaliwa na TRA iliyofanyika katika ukumbi wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Tanga (Tarecu) mjini hapa.

Alisema TRA kwa kushirikiana na ofisi ya mkuu wa wilaya, itaanza msako mkali dhidi ya wafanyabisha ambao hawana leseni za biashara kwa kuwa kufanya biashara bila leseni ni kosa kubwa la uhujumu uchumi.

Tumbo alisema msako huo kwa wafanyabiashara wasio na leseni utaanza keshokutwa kwa kupitia biashara zote ambazo hazina leseni ili hatua kali zichukulie dhidi yao.

Alisema mbali na msako wa wafanyabishara, pia msako huo utalenga wafanyabiashara wadogo, maarufu kama wamachinga, ambao hawana vitambulisho vya ujasiriamali.

Tumbo alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa na tabia ya kukwepa kodi kwa kutokuwa na leseni kitu ambacho kunasababisha kupungua kwa mapato ya serikali, hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya taifa.

Alisema mbali na msako huo pia kutakuwa na msako kwa kupita kwa kila mfanyabiashara kukagua mashine za risti za kielektroniki (EFD) kama zinatumika vizuri na atakayebainika hana mashine hiyo, ajue atachukuliwa hatua.

Kwa mujibu wa Tumbo, katika wilaya ya Muheza kuna miradi mingi ikiwamo ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya ambao serikali imechangia Sh. bilioni 1.5, hivyo miradi hiyo yote inahitaji fedha kutoka serikalini na kwamba wafanyabiashara wanatakiwa kuhakikisha wanalipa kodi ili itekelezwe.

Naye Meneja wa TRA Wilayani Muheza, Daudi Njohole, wafanyabiashara wanapouza bidhaa lazima watoe risti ambazo zitawasaidia pindi wanapokaguliwa na maofisa wa TRA, la sivyo mzigo huo utafahamika wa magendo.

Alisema wafanyabiashara wanapokuwa na changamoto za masuala ya kodi wasifunge maduka bali wafike ofisi za TRA kila Alhamisi ili kupata ufumbuzi katika biashara zao kwa kuwa kufunga biashara hakutatui tatizo lililopo.



Mchuuzi wa mananasi 'akiuchapa' usingizi wakati akisubiri wateja katika soko la Buguruni, jijini . **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Kamati ya Bunge yaipa tano hifadhi ya Mikumi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii imeupongeza uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kwa kuwa ni hifadhi pekee ambayo haina mgogoro wa mpaka kati yake na vijiji inavyopakana navyo.

Hatua hiyo inakuja ikiwa zimepita siku moja tu tangu Rais John Magufuli kuagiza uongozi wa wizara zote zinazohusika kusitisha kazi ya kuviondoa vijiji na vitongoji 365 vinavyodaiwa kuwa katika maeneo ya hifadhi.

Pia Kamati hiyo imeupongeza uongozi wa hifadhi hiyo kwa kupunguza matukio ya ujangili na majangili kudhibitiwa kwa kuwa katika mwaka 2017/2018 hadi sasa, hakuna tukio lolote la ujangili wa tembo lililotokea ndani ya hifadhi hiyo.

Akizungumza baada ya kusomewa taarifa ya hifadhi hiyo juzi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Nape Nnauye, alisema kitendo cha hifadhi kumaliza kutatua migogoro yote iliyokuwapo awali, ni jambo la kuigwa.

Nape alisema kuna haja ya hifadhi zingine kujifunza mbinu zilizotumiwa na hifadhi hiyo ili nazo zimalize migogoro hiyo na kuthibiti ujangili wa tembo.

"Hii si kawaida kukuta hifadhi haina mgogoro wa ardhi kati ya vijiji inavyopakana navyo. Hii kwangu ni hifadhi ya kwanza kuona haina mgogoro kabisa," alisema mwenyekiti huyo.

Katika hatua nyingine, Kamati hiyo iliipongeza Mikumi kwa kuwa ni hifadhi yenye idadi kubwa ya watalii wa ndani wanaoitembelea kulinganisha na watalii wa nje katika kipindi cha miaka mitano mfululizo ilhali hifadhi nyingi zimekuwa zikiongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watalii wa kutoka nje.

Awali, Mkuu wa Hifadhi hiyo, Godwell Meing'ataki wakati akisoma taarifa mbele ya kamati hiyo, alisema hifadhi hiyo imetatua migogoro iliyokuwapo awali pamoja na tatizo la ujangili wa tembo kutokana na ushirikiano uliopo kati ya vijiji, uongozi wa wilaya na kamati ya ulinzi na usalama.

Alisema mafanikio hayo yote yamepatika kwa kuchangiwa na vitu vingi ikiwamo ushirikiano, kufanya doria za mara kwa mara na elimu kwa wanavijiji kuhusu umuhimu wa kulinda hifadhi kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

## Shule binafsi yafutiwa usajili

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

SHULE ya Msingi ya Shinyanga Modern iliyoko mjini hapa, inayomilikiwa na mtu binafsi, imefutiwa usajili kutokana na kukosa vigezo vya kutoa elimu.

Uamuzi wa kuifuta shule hiyo iliyoanza kutoa elimu ya msingi tangu mwaka 2013, umefanywa kutokana na amri ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, kwa madai ya kutoa nyaraka za uongo, ikiwamo ukubwa wa eneo la shule.

Akizungumza juzi alipofanya ziara ya ukaguzi wa shule hiyo, Mboneko alibaini kuwapo kwa upungufu, hivyo kuagiza Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Mohamed Kahundi, kuifutia usajili na kuifunga.

"Shule hii haina vigezo vya kutoa elimu kwa watoto wetu. Kwanza mazingira yake ni machafu, madarasa hayana viwango, vyoo si rafiki kabisa havina hata mapaa juu. Eneo lake halikidhi vingezo vya kutolea elimu ya msingi na sijui usajili mlipataje," alisema Mboneko.

"Kutokana na upungufu huu uliojitokeza, kwanzia sasa ofisa elimu mkoa usajili wa shule hii ufutwe pamoja na kufungwa kutoendelea kutoa elimu ya msingi. Labda waendelee na chekechea na pia mmedanganya serikali ikiwa eneo linalopaswa kutolewa elimu linatakiwa ekari 4.5 na si 2.1," aliongeza.

Naye Kahundi, ambaye aliambatana na mkuu huyo wa wilaya, alisema awali walipokwenda kukagua shule hiyo, walipewa nyaraka zote pamoja na kuonyeshwa eneo lote la shule, huku wakitoa maelekezo ya makosa madogo madogo yafanyiwe ukarabati ikiwamo miudombinu ya majengo.

Alisema baada ya shule hiyo kupewa usajili na kuanza kutoa elimu, hakuna ukarabati wowote uliofanyika, huku eneo la shule ambalo awali walionyesha lenye ukubwa wa ekari 4.5 yalikuwa makazi ya watu na sasa wameshajenga nyumba zao. Aliahidi kutii maagizo ya kuifutia usajili.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Philip Okuku, akimwakilisha Mkurugenzi wa Shule hiyo, Titus Mwita, ambaye alikuwa nje ya mkoa wa Shinyanga, alikiri kuwapo na upungufu huo na kutolea ufafanuzi kuwa kwa sasa ndio wanafanya ukarabati wa shule na kuomba wapewe muda kwa kuwa kuendesha shule kunahitaji gharama kubwa.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe MWANGA WA JAMII

## *Dua, macho, masikio yaelekezwa kwa Simba*

**MABINGWA** watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam leo wanatarajia kushuka uwanjani mjini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kuwakabili wenyeji wao timu ya AS Vita.

Timu hizo zinakutana katika mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, zikiwa zimepangwa kwenye Kundi D.

Simba si wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano hayo ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), bali ni timu inayowakilisha klabu za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Simba ilianza vyema hatua hiyo ya makundi kwa kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Waarabu kutoka Algeria, JS Saoura na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa kundi hilo.

Wekundu wa Msimbazi ambao walikuwa nje kwa miaka 15 kwenye hatua hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika wanatakiwa kuendelea na kauli mbiu yao ya "YES WE CAN" huko ugenini na hatimaye wanaweza kuondoka na pointi tatu.

Nipashe inaamini kuwa ushindi unaweza kupatikana katika uwanja wowote na wachezaji wa Simba wanatakiwa kuondoa hofu ya neno ugenini.

Simba imekuwa ikicheza mbele ya mashabiki wengi, hivyo tunaamini kelele za mashabiki wa AS Vita na wadau wengine wa soka walioko Kinshasa hazitaweza kupunguza nguvu ya mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara.

Endapo Simba itafanikiwa kupata ushindi katika mechi ya leo, itakuwa imeendelea kujiweka katika njia nzuri ya kuelekea hatua ya robo fainali ambayo ni muhimu kwao baada ya awali kutinga hatua ya makundi.

Wachezaji wa Simba pamoja na benchi la ufundi wanatakiwa kufahamu timu zote zilizoingia hatua hiyo ya makundi ni nzuri, kinachotakiwa ni kuthibitisha kwamba hawakufika hapo kwa kubahatisha.

Nipashe inawakumbusha wachezaji wa Simba watakaopata nafasi ya kucheza mechi hiyo kufahamu huo ni wakati mwingine wa kutangaza vipaji vyao, kwa sababu mawakala kutoka sehemu mbalimbali duniani wanaifuatilia michezo hiyo ya juu katika ngazi ya klabu barani Afrika.

Huu ni wakati wa Watanzania kuacha tofauti na kuiunga mkono Simba ili iweze kutimiza maelekezo yaliyotolewa na Rais John Pombe Magufuli ya kutwaa taji la Afrika na kuachana na makombe madogo madogo ambayo wamekuwa wakiyachukua hivi karibuni.

Kila timu katika hatua hiyo ya makundi, inajipanga kuvuna pointi tisa kutoka katika mechi zake za nyumbani, lakini hilo halina uhakika hivyo, Simba leo inatakiwa kupambana na hatimaye kupata ushindi na kujiweka kwenye nafasi nzuri, huku pia ikiwapa furaha na heshima mashabiki na wanachama wake.

Nipashe linapenda kuwaombea kila la kheri Simba kwa sababu inaamini ushindi wao utaipa heshima Tanzania kwa sababu kila inapokwenda inatangaza jina la nchi.

Tunasema kuwa hakuna kisichowezekana, Simba ushindi ugenini unawezekana, wachezaji na benchi la ufundi wanachotakiwa ni kuendeleza kazi nzuri waliyoianza Januari 12 mwaka huu mbele ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





# Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## *Mpanga ratiba Ligi Bara atoke Ulaya?*

**KATIKA** hali ya kushangaza na kushtusha, Ligi Kuu Tanzania Bara imeingia katika mzunguko wa pili wakati baadhi ya timu bado hazijamaliza mechi zake za mzunguko wa kwanza.

Inawezekana kabisa hii ikawa ni ligi ya kwanza duniani kufanya hivyo.

Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB) na Shirikisho la Soka Nchini (TFF) ambao ndio wasimamizi wa ligi hiyo, msimu huu wameonekana kuwa na matatizo mengi kuliko wakati mwingine wowote ule.

Hakuna mtu anayekataa kuwa kuna baadhi ya vitu havikwepeki kama vile Simba kucheza mechi za kimataifa za Ligi ya Mabingwa Afrika karibuni kila wiki, hivyo viporo kwake haviepukiki.

Hapa Bodi ya Ligi inaweza ikakaa na kujitetea na kueleweka mbele ya wadau wa soka.

Lakini inakuwaje timu zinaanza mechi ya mzunguko wa pili kabla hazijamaliza mechi za mzunguko wa kwanza?

Nadhani timu zingesubiri kwanza Simba irejee halafu kila timu iliyokuwa ina kiporo chake dhidi ya Simba zicheze ndipo mzunguko wa pili uanze.

Cha ajabu zaidi ni kwamba hata Yanga na Azam zimenza kucheza michezo ya mzunguko wa pili wakati haijamaliza mechi baina yao wenyewe ya mzunguko wa kwanza, wakati klabu hizo mbili hazichezi mechi za kimataifa.

Baada ya michuano ya Kombe la Mapinduzi kumalizika huko Zanzibar, ilitegemewa timu hizo zipambanane na kumaliza mzunguko kwa kwanza, lakini sivyo.

Wakati ikitajwa tatizo la timu kucheza raundi ya pili kabla ya kumaliza ya kwanza ni ratiba ya Simba kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa, je mechi ya Yanga na Azam nayo tatizo ni nini?

Kwa nini imekwepeshwa wakati timu zote zipo na hakuna timu yoyote inayoshiriki michuano yoyote ile? Huu ni udhaifu mkubwa wa upangaji wa ratiba na kuisimamia.

Vyovyote vile watakavyojitetea Bodi ya Ligi, lakini ni kama msimu huu wameivuruga ligi kutokana na kuwa na ratiba ya kienyeji, isiyozingatia haki na usimamizi.

Mfano mwanzo tu wa ligi, tuliona Yanga ikipangiwa zaidi ya mechi sita mfululizo nyumbani, kitu ambacho hakijawahi kutokea kwenye historia ya soka Tanzania.

Nasema sita kwa sababu nazitoa zile ambazo ilihesabika kuwa inacheza ugenini, ingawa ilikuwa inacheza Uwanja wa Taifa na kama ukiunganisha na hizo, unapata mechi 11.

Hivi wapanga ratiba walikuwa wanashindwa kukwepesha mechi za ugenini na nyumbani?

Kwa nini timu ikicheza Dar es Salaam, ipangiwe tena na timu ambayo inatumia uwanja hapa hapa jijini?

Kingine ambacho kinaonekana wapanga ratiba wamefeli ni tangu mwanzo wa msimu, kuna baadhi ya timu kubadilishiwa uwanja.

Awali inaonekana mechi inatakiwa kuchezwa Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, lakini ghafla tunaambiwa inachezwa Dar es Salaam kwa sababu ambazo hazitolewi ufafanuzi wa kutosha, huku ni kufanya baadhi ya mashabiki waingiwe na wasiwasi.

Moja kati ya vitu ambavyo vinasababisha hata wadhamini wasite kuingia kujitokeza kudhamini Ligi Kuu Bara ni baadhi ya vitu kama hivi, ambavyo unaweza kuita ni ubabaishaji au "mipango michafu" inaandaliwa.

Wadhamini wanataka kuona ligi imara, ushindani, yenye uwazi, haki kwa kila timu, lakini pia ikifanana kwa usimamizi kama ligi nyingine duniani.

Ligi Kuu msimu huu si tu kwamba haina udhamini, lakini imekuwa ya kuchekesha kutokana na vitu nilivyovianisha hapa, kiasi kwamba imeshaanza kupoteza mvuto kwa wapenzi wa soka na kuonekana ni ligi ya kukamilisha ratiba.

Kwa wale wapenzi wa timu bado wanazifuatilia timu zao, lakini kwa wapenzi wa soka mvuto umeshaanza kupungua na hata kwenye "vibanda umiza" kwa kuangalia mpira mashabiki wengi wamepungua tofauti na ilivyokuwa awali.

Mashabiki wengi kwa sasa wanaonekana kujazana katika mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika au Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Cha kujiuliza haya yote yanayofanywa ni kwa makusudi, bahati mbaya, au utaalamu mdogo?

Kama ni utaalamu mdogo wa upangaji wa ratiba, je hakuna umuhimu wa kutafuta wataalamu nje ya nchi waje kutufundisha jinsi ya kupanga ratiba vizuri na kuisimamia bila kupindisha-pindisha mechi?

# Naibu Waziri awahenyesha maofisa ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

NAIBU Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, amewaonya wakuu wa idara za ardhi na ofisa ardhi mteule katika halmashauri za Mji Kibaha na wilaya za Kibaha na Bagamoyo mkoani Pwani kwa kushindwa kusimamia vyema majukumu yao.

Kutokana na hali hiyo, Mabula amewapa miezi miwili juzi watendaji hao kutekeleza maagizo waliyopewa ya kuingiza viwanja na mashamba kwenye mfumo wa malipo ya kodi ya ardhi kwa njia ya kielektroniki.

Sambamba na agizo hilo, wametakiwa wawe wametoa hati za madai kwa wadaiwa wote sugu na wasipotekeleza maagizo hayo ndani ya muda huo, watawajibishwa.

Mabula alitoa onyo hilo juzi alipofanya ziara ya kushtukiza katika halmashauri za wilaya za Bagamoyo, Chalinze na Kibaha kuangalia utekelezaji wa maelekezo aliyoatoa kuhusiana na ukusanyaji kodi ya ardhi, uingizaji wamiliki wa viwanja katika mfumo wa kielektroniki, utoaji hati za madai kwa wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi na kushughulikia migogoro ya ardhi.

Watendaji waliopewa onyo kali ni Mkuu wa Idara ya Ardhi katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Lucy Kimoi; Mjaliwa Mwamba, Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha; Mkuu wa Idara ya Ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Khalid Tumbulegen na Ofisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Gilly Simiyu .

Naibu Waziri alisema anashangazwa na watendaji hao kushindwa kusimamia sekta hiyo vizuri pamoja na kuwapo mfumo rahisi wa kufuatilia wamiliki wa viwanja na mashamba, jambo alilolieleza kuwa linaikosesha serikali mapato mengi yatokanayo na kodi ya ardhi.

Alisema pamoja na baadhi ya halmashauri kuonekana kuvuka zaidi ya asilimia hamsini ya makusanyo ya kodi ya ardhi hadi Desemba, mwaka jana, bado halmashauri hizo zina wadaiwa wengi wenye kiasi kikubwa cha fedha na kama kingekusanywa serikali ingepata fedha nyingi kupitia sekta hiyo.

Mabula alishangazwa na Halmashauri ya Mji Kibaha kushindwa kusimamia vyema utoaji hati za madai kwa wadaiwa wa kodi ya ardhi ambao kwa mujibu wa Kimoi, ilipeleka hati za madai kwa wadaiwa 10 tu wakati ina wadaiwa zaidi ya 200 jambo lililomfanya kuhoji ni vigezo gani vilitumika kupeleka hati za madai kwa wamiliki hao huku wengine wakiachwa.

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Mwamba alimweleza Mabula kuwa hakutoa hati hata moja ya madai kwa kuwa viwanja vingi katika maeneo hayo ni vipya na ni vigumu kuwapata baadhi ya wamiliki ili kuwapatia hati hizo.

Naibu Waziri Mabula alisema mji wa Kibaha kwa sasa unakua kwa kasi, hivyo watendaji wa sekta ya ardhi wanapaswa kuhakikisha wanaingiza katika mfumo viwanja na mashamba kufikia Machi 31 sambamba na viwanja vipya vitakavyopimwa na asingependa kuona halmashauri hizo zinashindwa kuviingiza kwa visingizio mbalimbali.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Mabula alikerwa na idara ya ardhi ilivyokalia hati za wamiliki wa viwanja bila kuwapatia wenyewe kwa visingizio mbalimbali ikiwamo kutokamilika taratibu za kupatiwa huku baadhi ya hati zikiwa katika ofisi hiyo kwa zaidi ya miaka miatatu.

Kutokana na hali hiyo, mabula aliagiza wamiliki wenye hati hizo watafutwe kwa kupigiwa simu ili kama kuna dosari wafahamishwe na kurekebishwa.

Pia alimwagiza mkuu wa idara ya ardhi katika halmashauri hiyo kuhakikisha anakamilisha hati hizo ndani ya miezi miwili na kuwapatia wamiliki vinginevyo atakumbana na rungu la kuondolewa katika nafasi hiyo.

# Watatu wafa maji, kujinyonga

**Na Steven William,** MUHEZA

WATU watatu wamefariki dunia katika matukio tofauti wilayani Muheza likiwamo la mtu mmoja kupoteza maisha kwa kuzama katika bwawa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alisema jana kuwa watu hao walifariki dunia katika ajali za majini na kujinyonga katika matukio tofauti na kwamba uchunguzi unaendelea juu ya vifo hivyo.

Alisema katika tukio la kwanza, katika eneo la utalii la Magoroto wilayani

hapa, mtu mmoja mkazi wa Dar es Salaam, ambaye hakufahamika jina lake mara moja, alifariki dunia juzi kwa kuzama katika bwawa la maji.

Katika tukio la pili, alisema Athumani Kanumba (50) mkazi wa kijiji cha Enzi wilayani Muheza, amefariki dunia baada ya kujinyonga na kwamba chanzo cha kujinyonga hakijafahamika.

Aidha, alisema katika tukio la tatu, Abdallah Mauya (22) mkazi wa kijiji cha Mgome, alifariki dunia baada ya kutumbukia katika kisima cha maji wakati akichota maji katika kijiji cha Kigongomawe kwa Anthony.

Kamanda Bukombe alisema marehemu hao wametambuliwa na ndugu zao na kwamba taratibu za mazishi zimefanyika katika maeneo yao ambayo wanaishi.



Mkuu wa wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko akikagua vyoo visivyo na ubora vya Shule ya msingi binafsi ya Shy. Moderm mjini humo juzi ambapo shule hiyo imefutiwa usajili kutokana na kukosa vigezo vya kutoa elimu hiyo ya shule ya msingi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mwanafunzi Sekondari Jitegemee apotea



**Na Mwandishi Wetu**

MWANAFUNZI wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Jitegemee jijini Dar es Salaam, Habiba Maduga (15) (pichani), anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka nyumbani kwao Manzese Tip Top.

Baba mzazi wa mwanafunzi huyo, Ibrahim Maduga, alisema jana kuwa mtoto wake aliondoka Desemba 15, mwaka jana, na kwenda kwa bibi yake, Zainabu Mussa, maeneo ya Manzese Uzuri lakini tangu hapo haijulikani alikokwenda.

"Tumefikisha tukio la kupotea kwake katika kituo cha polisi mpakani na kufungua jalada namba MMP/RB/1066/2018 na sasa tumekuja huku ili mtusaidie katika jitihada za kupatikana kwa mtoto wetu," alisema Maduga.

Ibrahim alisema mtu yeyote atakayemwona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi pia awajulishe kwa namba **0719-113818, 0684-525057 au 0788-326522.**

# Mamia wafurika kutoa maoni

INATOKA UK 3

wanadai utaratibu si mzuri wanataka waendelee kwa utaratibu wa zamani," alisema.

Kadhalika, alisema kuna kifungu kinazungumzia vyama vya ulinzi kwa chama cha siasa ambapo sheria hiyo inakwenda kuviondoa.

"Katika hili elimu ya uraia wengine wamesema ufanyike ukaguzi na msajili ndiye aratibu suala la utoaji wa elimu ya uraia isiwe kiholela bila kujua anachoenda kufundisha, sasa sisi tutapitia bishani zao zote kwenye maeneo haya na kuchukua ya msingi yanayofaa kwenye utungaji wa sheria," alisema.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, wako wanaosema vyama vya siasa havikutakiwa kusimamishiwa ruzuku zao wanapofanya ubadhirifu wakidai kuwa ni mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG), hivyo msajili asiingilie.

"Wengine suala la upatikanaji wa fedha kwa vyama vya siasa kutokana nje ya nchi wengine wanasema suala hilo vyama vitakufa," alisema.

Pia alisema kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya wadau kutoelewa vifungu na wengine kufika na mambo yanayozungumzwa kwenye mitandao na magazeti.

"Kwa kweli si hicho kilichoandikwa kwenye muswada, tunataka watu wanapokuja wawe wamesoma vizuri na kujua maudhui ya muswada,"alisema na kuwataka wadau wanapaswa kujikita kwenye ibara zinazotakiwa kufanyiwa marekebisho na vifungu vyake.

"Tumeendelea kutoa elimu hii maana kweli baadhi ya maoni hayaendani na vifungu vya ibara zinazofanyiwa marekebisho," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kuna wadau wametoa maoni yao kulinganisha na sheria za nchini Kenya na Ghana na kamati itachambua na kuangalia yanayofaa kutumia kwenye sheria hiyo.

"Wapo wadau wamefanya references ya utungaji wa sheria kwa nchi ya Kenya na Ghana kama mnavyojua ndio yenye demokrasia ya hali ya juu,"alisema.

Aidha alisema kuna wadau wanadai utungaji wa sheria unafanyika haraka na kwamba inahitajika muda zaidi jambo ambalo si kweli.

"Shehe Ponda kaja anasema mbona mnafanya haraka sheria hii inahitaji muda, najiuliza ni muda upi wakati mfumo wa vyama vingi ulianza muda mrefu miaka 27 iliyopita na sheria imekuwa ikifanyiwa marekebisho ambapo mara ya mwisho ilikuwa ni mwaka 2009 hadi sasa ni miaka 10.

"Hata muswada wenyewe tangu umesomwa mara ya kwanza hadi sasa ni miezi mitatu watanzania hawataki kujishughulisha kusoma,"alisema.

Aliwaomba Watanzania waendelee kujitokeza kutoa maoni na kwamba wao hawatayumba kwasababu ya fikra na maneno ya watu kwa kuwa wanaongozwa na kanuni.

Alisema Jumatatu na Jumanne, kamati itapitia michango ya wadau na kuona michango ipi inafaa kutunga sheria.



Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Prof. Tadeo Satta (kulia), akizungumza na wahitimu wakati wa Mahafali 12 ya Shahada ya Uzamili na Stashahada ya Uzamili katika Teknolojia ya Habari na Usimamizi wa Utalii, iliyotolewa na chuo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Avinashillingam Deemed cha India, yaliyofanyika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JMP amzungumzia mrithi nafasi yake

INATOKA UK 2

Alisema mkataba halisi wa mfumo huo ulifichwa na kipengele cha kutambua makusanyo ya fedha za kampuni za simu kilishaondolewa kwenye mkataba hivyo akatumia mbinu zake kukiongeza.

Rais alisema alipeleka muswada wa kuweka kipengele hicho ambacho kilifutwa na wajanja wakiwamo viongozi wa serikali waliokuwa na lengo la kuwaibia Watanzania.

Baada ya kupengele hicho kupitishwa, alisema walimwita mkandarasi kukamilisha mkataba wake na ulikamilika mwaka jana na jana aliukabidhi kwa serikali.

"Nawashukuru sana makandarasi walielewa nia yetu ilikuwa nini wakatimiza hivyo vipengele vyote na leo (jana) kazi imekamilika," alisema Rais Magufuli.

Alisema mbali na mtendaji huyo, yuko mwanamke ambaye alitishwa hadi kufikia hatua ya kuitwa mfuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

"Nimemtoa Dk. Simba, lakini mafanikio ya Sh. bilioni 93 yaliyopatikana tangu kuazishwa kwa mfumo huu wa TTMS hata senti tano sijapewa, zinaenda kwa Watanzania na hiyo ndiyo huduma kwa wananchi," alisema.

Alimtaka mfanyakazi wa TCRA aliyeitwa mamluki wa Chadema, afanye kazi kwa bidii kwa sababu kinachoangaliwa kwenye kazi ni utendaji na si chama.

Alisema pia wapo watumishi ambao ni wafuasi wa CCM lakini ni wezi na kila siku wamekuwa wakitembea na mavazi ya chama.

"Wizi hauna dini, hauna chama, wachungaji hawa wanahubiri neno la Mungu kila siku hadi wanalia, lakini utakuta mwizi yupo kanisani na anatoa sadaka na kuondoka kimya kimya na serikalini kuna mchanganyiko wa watu kama hao," alisema Rais Magufuli.

Kuhusu mafanikio ya kufungwa kwa mfumo huo, Rais Magufuli, alisema umewezesha TCRA kukusanya Sh. bilioni 93.65.

Alisema mbali na mafanikio changamoto zilizopo ni kutokana na kuongezeka kwa kasi ya teknolojia ya mawasiliano nchini ni kusababisha kuadhirika kwa baadhi ya mila na desturi na kushuka kwa maadili ya jamii mbalimbali.

Pia alizisihi taasisi za umma ambazo hazijajiunga na mfumo huo zifanye hivyo mara kwa sababu kati ya taasisi 667 ni 339 zilizounganishwa.

**KILABA AULA TENA**

Rais Magufuli pia alimuongezea miaka mitano ya kuendelea kuwapo kazini Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Mhandisi James Kilaba kutokana na kuridhishwa na utendaji kazi wake.

Awali, Mhandisi Kilaba alimweleza Rais Magufuli kuwa mamlaka hiyo ilianzishwa mwaka 2003 kwa lengo la kutoa leseni kwa ajili ya utangazaji.

Kilaba alisema mfumo ulianza rasmi Oktoba Mosi, 2013 na Septemba 30, mwaka jana, ulikamilika rasmi na jana ulikabidhiwa kwa TCRA.

Alisema faida za mfumo huo ni kubaini mambo mbalimbali ikiwamo mawasiliano ya simu ya ulaghai na utahakiki mapato ya watoa huduma za mawasiliano.

"Kama mnavyojua shughuli za kiuchumi zinazohusiana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), zimeongezeka na zinaendelea kuongezeka kwa kasi kubwa katika nchi yetu na hivyo kuhitajika kuwapo na mifumo mahiri ya usimamizi," alisema Mhandisi Kilaba.

Aliongeza kuwa "Matamanio yetu kuwa Tehama iendelee kusaidia katika sekta nyingine kukuza uchumi wa nchi,"

Aidha, alisema mfumo huo utawezesha upatikanaji wa takwimu za mawasiliano ya simu yatakayofanyika ndani na nje ya nchi.

Alisema mfumo huo utakuwa unagundua mawasiliano ya simu ya ulaghai, kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandaoni na kusimamia kwa ufanisi ubora wa huduma za mawasiliano na hivyo kuboresha viwango vya huduma.

Faida nyingine, kwa mujibu wa Kilaba, ni kutambua taarifa za laini ya simu, kubaini na kufungia simu zenye namba tambulishi zilizonakiliwa na kutoa takwimu zinazohusiana na matumizi ya huduma za mawasiliano.

## RC aingilia kati

INATOKA UK 2

wakashikana mashati na kuanza kutwangana makonde.

Alipotafutwa kuzungumzi tukio hilo, Mkuu wa Wilaya hiyo (Mbogho) alisema hana taarifa lakini akaomba apewe muda wa kufuatilia kujua usahihi wa taarifa hiyo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Lubuva alipoulizwa kuhusiana na taarifa za kuhitilafiana na ofisa huyo na kisha kupigana, alisema anaiachia mamlaka husika ifanye kazi yake.

Desemba 22, mwaka jana, Jafo na Mkuchika walifika mkoani Kilimanjaro kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa la kuwataka kumaliza tofauti za wateule hao.

## Wagonjwa 19

INATOKA UK 2

(ICU) kwenye hospitali mbalimbali.


Aidha, alisema katika kipindi cha Julai na Desemba, mwaka jana, Muhimbili ilitoa huduma za kupandikiza vifaa vya usikivu kwa watoto 11 na kufikisha jumla ya watoto 21 waliopata huduma hiyo toka ilipoanza Juni, 2017, jambo lililosaidia kuokoa zaidi ya Sh. milioni 840 ambazo zingetibu watoto 21 nje ya nchi.

"Kabla ya hapo huduma hii ilikuwa inapatikana nje ya nchi kwa gharama kati ya Sh. milioni 80 mpaka 100 kwa mtoto mmoja, huku Hospitali ya Taifa Muhimbili gharama ni Sh. milioni 35 mpaka 40," alisema Waziri Ummy.

Wakati akijibu maswali ya wajumbe wa kamati hiyo, ambao ni wabunge, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema kuwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), imefanya upasuaji kwa wagonjwa 211.

Alisema kati ya wagonjwa waliofanyiwa upasuaji, watu wazima walikuwa 89 na watoto 60, huku watu wazima 62 wenye matatizo kwenye mishipa ya damu walifanyiwa upasuaji wa mishipa ya damu.

Aidha, Dk. Ndugulile alisema wagonjwa 521 walipatiwa matibabu ya upasuaji wa moyo kupitia tundu dogo kwa upande wa mtambo maalum (catheterization laboratory).



# Halmashauri yaunda kikosi kazi maalum kusaka wakwepa kodi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha imeunda kikosi maalum kitakachofanya operesheni ya kushutukiza ya kukusanya kodi ya serikali nyumba kwa nyumba kwa wafanyabiashara wakwepaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Mkurugenzi mtendaji wa halmashauri hiyo, Dk Maulid Madeni, alisema hatua hiyo wameifikia baada ya kubaini kuwapo kwa wafanyabiashara wanakwepa kulipa kodi ya serikali.

Alisema watakaobainika kukwepa kodi ya serikali watachukuliwa hatua za kisheria.

"Operesheni hii inalenga kukusanya kodi na kuongeza mapato ya jiji lakini tukimbaini mfanyabiashara yeyote amekwepa kulipa kodi ya serikali tutamchukulia hatua kali za kisheria," alisema.

Alisema operesheni hiyo ilianza juzi na itawalenga wafanyabiashara wa maduka, wenye viwanda na wamiliki wa nyumba za kulala wageni ambao wanadaiwa kuwa vinara wa kukwepa kulipa kodi katika Jiji la Arusha.

Aliongeza lengo la operesheni hiyo ni kuhakikisha Jiji la Arusha linafikia malengo na kuvuka makadirio ya makusanyo ya Sh. bilioni 15 iliyojipangia kwa mwaka, ili fedha hizo zitumike kupeleka maendeleo kwa wananchi kama ilivyokuwa madhira ya serikali.

Aidha, alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara katika Jiji la Arusha wamekuwa wakikiuka sheria, kanuni na taratibu za nchi kwa kushindwa kutekeleza wajibu wao wa kulipa kodi.

"Serikali imewaamini watendaji wake ni maana tumepewa dhamana ya kusimamia ndio maana tuna mpango wa kutoka nje ya ofisi zetu kuwasaka wafanyabiashara vinara wa kukwepa kulipa kodi ya serikali ambapo ni wajibu wao wa kikatiba," aliongeza.



Mkazi wa jiji akikokota guta lake lililosheheni matenga matupu katika eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana, jambo ambalo ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# EAC yalaani shambulio la kigaidi nchini Kenya

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

JUMUIYA ya Afrika Mashariki, (EAC), imelaani shambulio la kigadi lililotokea katika Hoteli ya Dusit D2 ambalo limeua watu 14 na kujeruhi watu kadhaa.

Katika salaamu zake za rambirambi kwa Rais Uhuru Kenyatta jana, Katibu Mkuu wa EAC, Balozi Liberat Mfumukeko, alisema shambulio hilo halivumiliki.

"Tumepokea kwa masikitiko na mshtuko mkubwa kwa shambuli hilo la kigaidi lililotokea Januari 15, mwaka huu ambapo watu 14 wamethibitishwa kufariki dunia.

"Kwa niaba ya EAC na kwa niaba yangu mwenyewe, natuma salamu hizi za rambirambi kwa watu waliofariki na tunawaombea waliojeruhiwa kupona haraka," alisema.

"Nachukua fursa hii kulaani kwa nguvu zote shambulio hilo la kigaidi na kamwe halivumiliki kwani limeua watu wasio na hatia, kuwajeruhi na kusababisha machafuko katika nchi inayothamini ustaarabu," alisema.

# Longido wazindua ujenzi wa hospitali ya wilaya

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

MKUU wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, amezindua ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo Serikali Kuu imetoa Sh. bilioni 1.5 kukamilisha ujenzi wake.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Longido, imesema itachangia Sh. milioni 300 kutoka kwenye mapato yake ya ndani.

Katika uzinduzi huo uliofanyika jana, Mwaisumbe na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Juma Mhina, walishiriki kuchimba shimo la choo kwa ajili ya hospitali hiyo.

Wakizungumza katika hafla hiyo, Diwani wa Viti Maalum, (Chadema), Naomi Mollel, alisema kujengwa kwa hospitali hiyo kutapunguza vifo vya wanawake, wajawazito na watoto. Mkazi wa Longido,

Mary Kashuma, alisema hospitali iliyokuwa ikitumika hapo awali kama ya wilaya, ilielemewa. "Kipekee ninamshukuru Rais John Magufuli kwa kutukumbuka wana Longido, naona na maji nayo yameshafika bado tu kuanza rasmi kutumika,

Mungu ambariki Rais wetu," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya, Mwaisumbe, alisema Serikali Kuu imetoaSh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo, lakini bado hazitoshi.

Alisema kazi kubwa ya wananchi ni kusaidia kuchimba msingi, mitaro, kubeba mawe pamoja na mbao kwa kufanya hivyo kutasaidia kuokoa gharama na fedha itatumika kwa bajeti hadi kukamilisha ujenzi, hivyo wananchi jitokezeni.

Alisema alitoa agizo kwa mkandarasi anayejenga hospitali hiyo kuhakikisha anajenga kwa muda ulipangwa na kwa kuzingatia viwango.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Juma Mhina, alisema halmashauri itachangia Sh. milioni 300 katika ujenzi huo kutoka kwenye mapato ya ndani kadri watakavyokusanya fedha.

Alisema wilaya hiyo ina miaka 11 tangu kuanzishwa kwake lakini haijawahi kuwa na hospitali ya wilaya huku ikiwa na wakazi zaidi ya 142,000, kata 18 huku kilomita za mraba zikiwa ni 7,782.

Aliongeza kuwa fedha hizo ni sehemu ya kuanza majengo saba, lakini ataendelea kuhamasisha wananchi kujitokeza kuchangia kwa chochote. "Tunafahamu tupo kwenye lango la mpakani mwa nchi ya Kenya, hivyo nategemea hospitali hii itahudumia raia wa nchi mbalimbali wakiwemo Sudan Kusini, Uganda, Kenya, Ethiopia na Rwanda.

"Kubwa zaidi niombe serikali sikivu ya Rais Magufuli, pindi hospitali hii itakapo kamilika watulete watumishi wazoefu na wenye weledi na kazi yao watakao hudumia wananchi haya wenye uhitaji wa huduma katika hospitali yao," alisema.





# RC Mghwira awataka wauza mitumba kukaa mguu sawa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira amewataka wafanyabiashara wa nguo za mitumba katika soko la Kumbukumbu ya King George maarufu kama Meimoria kujiandaa kisaikolojia kuhamishwa kuanzia sasa, baada ya serikali kutoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa michezo.

Alitangaza uamuzi wa serikali wa kuwaondoa wafanyabiashara hao jana, wakati akizungumza na wadau wa sekta ya utalii na wanamichezo katika uzinduzi wa mashindano ya kimataifa ya riadha ya Kili Marathon.

"Tumewaandaa wafanyabiashara kuondoka Meimorial, tumeipa mamlaka Manispaa ya Moshi kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wetu hawatanyanyaswa, hawatasumbuliwa na watapangiwa masoko mengine yaliyopo ndani ya Manispaa na sisi wananchi tutatangaziwa.

"Tutataka kuambiwa kwamba nguo za mitumba zinauzwa sehemu fulani, bidhaa nyingine zinauzwa wapi na kama kawaida tutafuata biadhaa mahali zilipo. Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya (Kippi Warioba) na Meya (Raymond Mboya) mko hapa, kuanzia sasa mji wa Moshi upangike, ueleweke na hasa katika maeneo ya biashara, nimekuwa mkali kiasi kwenye suala la biashara ya vyakula na masoko kama manne, matano hivi."

Mwaka 2007, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi iliamua kulifunga soko la Kiboriloni lililokuwa linawapa huduma wananchi wa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na hata nchi jirani na kuwahamishia wafanyabiashara hao wa mitumba katika Uwanja wa Memoria.

Alisema tayari Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imeahidi kuingiza fedha za awali za kuanza ujenzi wa uwanja huo kiasi cha Sh. milioni 500 na serikali ya mkoa nayo inakusudia kuwaita mezani mwezi huu, wadau wa maonyesho ya utalii ya kimataifa ya Kili Fair na wanamichezo kutoka Kili Marathon kuwachangisha zaidi ya Dola 500,000 za Marekani.

Akizungumza na wadau hao, Dk. Mghwira alionyesha kukerwa na wafanyabiashara kuzagaa katika maeneo yasiyo rasmi akisema: "Bidhaa zimezagaa mpaka barabarani, wageni wanapenda sana kununua vitu vyetu kwa sababu ni vya asili na havina dawa nyingi na wengine wanatoka mbali hasa hoteli kubwa kuja kuchukua bidhaa kutoka kwetu. Naomba utaratibu huu utengenezwe vizuri, Kili Marathon na Kili Fair zote zinaleta zaidi ya wageni 12,000 hadi 15,000 kwa wakati mmoja."

Alisisitiza kuwa pamoja na mambo mengine, watalii wanapokuja kupanda mlima Kilimanjaro wanatembelea masoko ya Moshi, hivyo ni vyema ustaarabu ukaonekana kila mara.



Gavana wa Klabu ya Lions District 411C, Mustafa Kudrati (wa nne kushoto), akitoa zawadi ya kompyuta mpakato (Laptop) kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, Michael Mwandezi, ikiwa ni sehemu ya kupongeza kwa baadhi ya shule za Manispaa zilizofanya vizuri katika mitihani ya taifa. **PICHA: JAMES LANKA**

# Makachero wadaka samaki waliokuwa wanatoroshwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KIKOSI maalumu cha makachero wa Jeshi la Polisi mkoani Kilimanjaro, kimekamata ndoo 180 za samaki waliopigwa marufuku kwa matumizi, wakiwa wanatoroshwa kuelekea mkoani Tanga. Samaki hao wachanga walivuliwa kwa njia haramu usiku wa manane juzi katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, licha ya kuwapo kwa vikosi vya serikali vinavyoendesha operesheni mbili za kitaifa za Jodari na Sangawe.

Taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Hamisi Issah imesema kuwa samaki hao walikamatwa usiku huo huo katika eneo la Mazinde, Wilaya ya Korogwe, baada ya Polisi kufukuzana na magari mawili yaliyokuwa yamebeba samaki hao. "Polisi wakiwa doria majira ya saa 7:45 usiku katika Kata ya Kiria, Wilaya ya Mwanga waliyaona magari mawili aina ya Toyota Pick Up na kuyatilia shaka na walipowafuata walianza kukimbiza magari na ikawalazimu Polisi kuwafukuza hadi walipowakamata na kuwapekua.

Zaidi aliongeza: "Walipowapekua walikuta Toyota Pick Up nyeupe yenye namba za usajili T 817 AXY iliyokuwa ikiendeshwa na dereva Rajab Mndeme ikiwa na ndoo 85 za samaki wachanga na gari la pili Toyota Hilux nyeusi, T 327 BEB inayoendeshwa na Almasi Shekigenda nayo ikiwa na ndoo 95 za samaki hao."

Katika purukushani hiyo ya kufukuzana, dereva Almasi Shekigenda alifanikiwa kutoroka na kutelekeza gari lake, lakini Polisi waliweza kumdhibiti na kumkamata dereva Rajab Mndeme ambaye kwa sasa anashikiliwa katika Kituo Kikuu cha Polisi Mwanga.

Mwaka jana, serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitangaza kuanzishwa kwa operesheni mbili za kitaifa zilizopewa jina la Sangawe na Jodari ambazo zinalenga kuwabana wavuvi haramu wanaoangamiza mazalia ya samaki katika mabwawa, maziwa, mito na ukanda wa bahari hindi.

Kabla ya kuanza kwa oparesheni hizo, serikali ilitoa muda kwa wavuvi haramu wanaovua mazalia ya samaki kwa kutumia makokoro katika Bwawa la Nyumba ya Mungu na maeneo mengine nchini kuwasilisha nyavu hizo kwa serikali za vijiji.

Aidha, vyanzo zaidi vya taarifa vinaeleza kuwa makokoro na nyavu ndogo katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, bado ni kitendawili kwa vile wavuvi wengi wanakiuka Sheria Namba 22 ya Mwaka 2003 inayowataka kufanya uvuvi unaokubalika kisheria.

# Wadau waomba elimu uchunaji ngozi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAKATI serikali ikijipanga kuingia katika uchumi wa viwanda wadau wa sekta ya ngozi wameombwa kutoa elimu juu ya uchunaji ngozi ili bidhaa hiyo ilete tija kwa wafugaji.

Imeelezwa kuwa baadhi ya wachunaji wa ngozi hawana elimu ya kutosha kuhusu namna ya uchunaji ambao huharibu ngozi na kuifanya ikose soko.

Mkurugenzi wa kiwanda cha ngozi cha Himo Tanaries (HITA), Sabas Woisso alisema kuwa kumekuwepo na changamoto kubwa katika zoezi zima la uchakataji wa ngozi ambazo zinachangia kushuka kwa bei ya bidhaa hiyo kila mwaka.

Aidha, Woiso aliongeza kwa kuwa wanatarajia kuingia katika uchumi wa viwanda, ni lazima kuhakikisha kuwa wanakuwa na malighafi nzuri na za kutosha.

"Sasa tunaelekea katika uchumi wa viwanda ni lazima tuhakikishe kuwa ngozi ambazo tutazitumia katika nchi yetu kuzalisha bidhaa mbalimbali zinakuwa na ubora ili soko letu liweze kuwa la kimataifa na tuweze kufahamika zaidi na ndio maana nasema wadau wa sekta ya ngozi huu ndio muda muafaka wa kujipanga katika hili, "alisema Woiso

Kwa mujibu wa Woisso bado kuna uelewa mdogo kwa wafugaji kutunza ngozi za wanyama ili ziweze kuwa na bei katika soko la dunia.

"Ng'ombe unakuta wanapigwa chapa sehemu zisizo maalumu au unaenda mchinjioni unamkuta mchunaji kalewa chakari anatoboa toboa ile ngozi bila sababu yoyote ile sasa hii inashusha thamani ya ngozi,"alisema Woiso.

Katika hatua nyingine Woiso aliitaka serikali kujenga mikakati katika kuinua sekta ya ngozi hapa nchini ikiwemo kuwajengea uwezo juu ya kutengeneza bidhaa za ngozi sambamba na utafutaji wa masoko.

Alisema kinachofanyika hivi sasa kwa watengenezaji wa bidhaa za ngozi ni kujitafutia elimu wenyewe au kulazimika kutafuta wataalam nje ya nchi kitu ambacho bado ni gharama kwa wazalishaji hao na hivyo jambo hilo lingeweza kufanyika kwa ubiana serikali.

Woiso aliishukuru serikali ya awamuya tano kwa jitihada ambazo imeonyesha kwa kusisitiza kununua bidhaa za ndani kwani kwa kufanya hivyo ni kufanya wajasiriamali wa ndani kuweza kukuza mitaji yao tofauti na kuendeleza kuagiza kutoka nje ya nchi.

"Wakati umefika kwa halmashauri na Mkoa uwatumie wataalamu waliopo katika mikoa hiyo kutoa elimu juu ya uchinjaji bora na kuboresha machinjio yaliyopo katika kuweka miundombinu rafiki ikiwemo taa,"alisema Wiliam Mlay.



HABARI DODOMA

# RC ashauri wakulima waje kivingine kuongeza uzalishaji

**Na Elisante John,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi amewataka wakulima wa zao la alizeti kuzingatia ushauri wa maofisa ugani, ili kufikia lengo lililokusudiwa na serikali la kujitosheleza kwa mafuta ya kula nchini.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati wa kukabidhi tani tano za mbegu ya alizeti aina ya record, zinazozalishwa na Agricultural Seed (ASA) ya Arusha, kwa vyama vya ushirika tarafa ya Mtinko, Singida vijijini.

Alisema kutokana na hitaji kubwa la mafuta ya kula, lazima wakulima wabadili mbinu za kilimo kwa kufuata ushauri wa wataalamu na kupanda mbegu zitakazoongeza mavuno ili kutosheleza mahitaji ya viwanda katika Mkoa huo na nchini kwa ujumla.

Dk. Nchimbi, alisema mbegu hizo zinazosambazwa na N & N Trading Co. Limited ya mkoani Dodoma, kama mkulima atafuata masharti, ekari moja itazalisha magunia 10 hadi 12.

Alisema kama wakulima watatumia mbegu zingine walizozoea watapata magunia manne.

Aidha Dk. Nchimbi alisema lengo na mkakati huo ni kuona viwanda vya kukamua mafuta ya alizeti katika mkoa huo vinafanya kazi muda wote wa mwaka, ili kuinua uchumi wa jamii, mkoa na taifa kwa ujumla.

Aliwaonya watakaohujumu kwa nia ya kudhoofisha juhudi za kuongeza mavuno ya alizeti, katika mkoa wa Singida watachukuliwa hatua.

Akipokea mbegu hizo, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Tumaini Mudida Mahamoud Nkuhi, aliishukuru serikali, benki ya maendeleo ya wakulima (TADB) juu ya mkopo kwa chama chake, hadi kupatikana kwa mbegu hizo.

"Kwa niaba ya wakulima wa Tumaini Amcos, nakushukuru sana wewe RC na benki ya TADB kwa mbegu hizi...tangu nianze kufuatilia, wakulima wangu wananipigia sana simu, nilipowaeleza nimefanikiwa, wamefurahi sana," alisema Nkuhi.

Naye, Mkurugenzi wa N & N Trading Co. Limited ya Dodoma Said Mhalule, aliwataka wakulima kuzingatia masharti na kanuni bora za kilimo ili mbegu hizo ziweze kuongeza mavuno ya alizeti, hivyo kuinua uchumi wao na taifa.

Alizeti ni mojawapo ya mali ghafi inayochakatwa katika viwanda 144 vya mafuta ya kula mkoani Singida ambapo msimu uliopita wa 2017/18 tani 97,757 zilivunwa huku msimu huu matarajio yakiwa ni kupata tani 216,406, wakati mahitaji ya viwanda ni tani 482,500.



Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Makame Mbarawa (wa pili kulia), akitoa maelekezo kwa mafundi wanaochimba mtaro wa bomba kuu la maji yatakayotumika kwenye majengo yanayojengwa mji wa kiserikali uliopo Mtumba, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mkumbo ahimiza mazingira bora kwa wafanyakazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya maji Profesa Kitila Mkumbo amewataka viongozi wa serikali kuweka mazingira mazuri kwa wafanyakazi wao ili wafanye kazi kwa uadilifu.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo juzi wakati wa hafla fupi ya kumpongeza Mfanyakazi bora wa Wizara ya Maji Heriel Msangi, kwa mwaka 2018.

Alisema viongozi mbalimbali katika sekta za umma wamekuwa wakiwalalamikia wafanyakazi wao kuwa hawafanyi kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi bila kujali mazingira ambayo wamewawekea.

"Viongozi wengi tumekuwa na tabia ya kuwalalamikia watumishi wetu kuwa sio wafanyakazi bora bila kujali namna ambavyo tunawawekea mazingira katika ufanyaji kazi wao wa kila siku...

"Kijana huyo ambaye leo tunampongeza angekuta viongozi wake wa ngazi za juu hawamfutilii na kumsaidia katika kutetea maslahi ya nchi asingeweza kufanikiwa katika hili ambalo leo tunamapongeza"alisema.

Alisema wafanyakazi wamegawanyika katika makundi matatu ambayo kiongozi anatakiwa kuyatambua ili aweze kusimamia na kuleta tija katika taasisi yake.

"Asilimia 25 ya wafanyakazi hawa ni wale ambao ni wazuri wakati wote wanafanya kazi bila kusukumwa wala kuwekewa sheria za kuwabana lakini wapo asilimi 50 hawa ni wale ambao ni wafanyakazi wazuri lakini wanweza kubadilika wakati wowote kama hauta weka njia za kuadhibiti lakini asilimia 25 ya mwisho ni wale ambao wanafanya kazi kwasabau ya sheria zilizopo,"alifafanua Prof. Mkumbo

Aidha alisema kuwa Wizara yake hivi sasa ina jukumu kubwa ambalo imepewa na Rais la kupitia upya sheria za rasilimali za maji pamoja na kanuni zake.

"Hii kazi tumepewa na Mheshimiwa Rais na hatuna muda hata wa mwezi mmoja kukamilisha hili tunatakiwa kutengeneza sheria ambazo hazita muumiza mtu wala mtu kuumiza rasilimali zetu za maji zilizopo,"alisema.

# Serikali za mitaa kinara kwa rushwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(Takukuru) mkoani Dodoma imepokea jumla ya taarifa 139 za vitendo vya rushwa na makosa mengine huku serikali za mitaa zikiongoza katika kipindi cha Oktoba-Desemba 2018.

Kwa mujibu wa taarifa ya utendaji kazi iliyotolewa jana kwa waandishi wa habari na Naibu Mkuu wa Taasisi hiyo jijini Dodoma, Musa Chaulo, katika kipindi hicho uchunguzi wa majalada 13 yalikamilika na kufunguliwa kesi mpya 3 Mahakamani.

Aidha, alisema katika taarifa zilizopokelewa, Serikali za Mitaa iliongoza kwa tuhuma 43, Idara ya Afya 18, Mahakama 18, Mabaraza ya Kata 17, Elimu 14,Polisi 12, Maji 8 na 9 zilizosalia zinahusu Vyuo vya Elimu ya Juu, Mashirika ya Umma, mifugo na viongozi wa kisiasa.

"Tuhuma zisizo za rushwa zilihamishiwa kwenye Idara husika, pia Takukuru Dodoma imejipanga kuendelea na kazi za kuzuia na kupambana na rushwa kwa robo hii ya tatu, ambapo pamoja na kazi nyingine itajikita katika kufuatilia matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo ili kuhakikisha fedha za serikali na wafadhili hazipotei na thamani halisi ya fedha inapatikana,"alisema.

Aidha, alisema taasisi imefanya uchambuzi wa mifumo mbalimbali ili kubaini mianya ya rushwa na kushauri namna bora ya kuondokana nayo ili kudhibiti vitendo vya rushwa.

"Uchambuzi umefanyika mara tisa katika idara za ulinzi, Halmashauri, Afya, Mawasiliano, Umwagiliaji, na Manunuzi. Warsha sita zimefanyika katika idara ya elimu, ulinzi, Maji na Ardhi,"alisema

Alisema matumizi ya fedha za miradi 20 ya maendeleo yenye thamani ya Sh.Bilioni 44.669 imefuatiliwa ili kuhakikisha fedha za miradi ya maendeleo zinatumika vizuri kama iliyopangwa na zinatumika kwa wakati.

"Miradi iliyofuatiliwa ni miradi miwili) ya ujenzi yenye thamani ya Sh.Bilioni 35.464, miradi ya maji tisa yenye thamani ya Sh.Bilioni 6.31,miradi ya afya miwili yenye thamani ya Sh.milioni 900, Mradi wa barabara mmoja wenye thamani ya Sh.milioni 700,"alisema.

Pia alisema miradi mitatu ya mifugo yenye thamani ya Sh.Milioni 678.9 na miradi mitatu ya elimu yenye thamani ya Sh. milioni 636.4.

"Katika miradi hiyo iliyofuatiliwa uchunguzi umeanzishwa katika miradi ya maji na elimu,"alisema.

Alitoa rai kwa wananchi wote, watumishi wa sekta ya umma na binafsi, kujiepusha na vitendo vya rushwa kwa kuwa ni kinyume na maadili.

# Waziri ataka wamiliki hoteli za kitalii wasiagize kuku nje

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Maliasili, Uvuvi na Mifugo, Rashid Ali Juma amesema kuwa umefika wakati wa kuwahamasisha wamiliki wa hoteli za kitalii kununua kuku wa hapa nchini badala ya kuagiza kutoka nje.

Aliyasema hayo jana baada ya kukagua mradi wa ufugaji wa kuku kwa ajili ya vijana wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Alisema kuwa Zanzibar ina uwezo wa kuzalisha kuku na kuachana na kutegemea wanaoagizwa kutoka nje ya nchi.

Aliongeza kuwa kuku wanaoagizwa Zanzibar kutoka nje ya nchi hawana uhakika wa usalama kwa matumizi ya binadamu.

"Hatujui kuku hao wamechinjwa lini na wanatumia muda gani kusafirishwa hadi kufika Zanzibar "alisema Rashid.

Aidha, alisema kuwa ni vyema kudhibiti soko la kuku na kuhakikisha kuku wanaouzwa wanazalishwa Zanzibar na wawe wamekomaa.

Alisema ufugaji wa kuku utaweza kukidhi mahitaji ya ajira kwa vijana na kuondokana na dhana ya kuajiriwa serikalini.

Aliongeza kuwa Zanzibar inawimbi kubwa la vijana wasio na ajira na wamekuwa wakihitimu vyuo vikuu kwa wingi wakati upo uwezekano wa kuwa na ajira binafsi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud alisema mkoa wake umeanzisha mradi huo ili kuwawezesha vijana katika ufugaji wa kuku.

Alieleza kuwa matumaini yake mradi huo utapunguza kilio kikubwa cha vijana katika suala la ukosefu wa ajira.

Kwa upande wake msimamizi wa mradi wa vijana wa ufugaji wa kuku,Rashid Othman alieleza kuwa kuku wanaowafuga hawatumii madawa wala kemikali.

"Huu ni ufugaji hai Ogarnic ambao hautumii madawa ya aina yoyote "alisema.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Ussi Gavu (wa pili kulia), akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, katika mkutano uliofanyika katika Ofisi ya Rais Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wafanyakazi waomba eneo ujenzi wa kiwanda

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAFANYAKAZI wa kiwanda cha Chakko kinachojishughulisha na utengenezaji na urejeshaji wa matumizi ya bidhaa za plastiki na vigae wameiomba serikali ya Mkoa wa Mjini Magharibi kuwapatia eneo ili wajenge kiwanda.

Walieleza hayo mbele ya Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud kiwandani hapo kuangalia shughuli zinazofanywa hapo.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wenzake, Khamis Juma alisema kwa sasa eneo wanalofanyia shughuli zao haliendandani na kazi wanazozifanya jambo ambalo linalosababisha kupungua ufanisi wa utendaji kazi zao.

Alieleza imekuwa kero kwa wakaazi wa karibu wa eneo hilo kutokana na kiwanda kipo karibu na makaazi ya watu.

Aidha, alieleza kuwa kazi wanazozifanya zimekuwa na tija kubwa katika kujiendeleza kimaisha wao na familia zao licha ya changamoto hiyo ya udogo wa eneo la kufanyia shughuli zao.

Alisema shughuli wanazozifanya zinaendana na suala la kimazingira pamoja na kuunga mkono jitihada za serikali za Tanzania ya Viwanda. Akizungumza na viongozi na wafanyakazi wa kiwanda hicho, Mahmoud alisema, ameridhishwa na kazi zinazofanywa kiwandani hapo kwa kuwa kinasaidia kuongeza ajira.

Aliahidi kushirikiana kwa karibu na uongozi wa kiwanda hicho katika kuwatafutia eneo ambalo litakidhi mahitaji ya shughuli zao na kupelekea kuongeza udhalishaji wa bidhaa zao pamoja kutanua wigo wa ajira kwa wananchi wa mkoa huo na Zanzibar kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Seleiman Ali Mohammed, alisema pamoja na changamoto ya eneo inayoikabili taasisi yake, lakini kiwanda hicho kimeweza kutoa fursa za ajira kwa vijana wengi ikiwa ni pamoja na kuwapatia taaluma ya ujasiriamali kwa watu walio nje.

# Waziri abariki mitihani kidato cha pili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma amesema ameridhishwa na usimamizi wa mitihani ya kidato cha pili inayofanyika Unguja na Pemba.

Waziri huyo alisema hayo baada ya kufanya ziara ya kutembelea wanafunzi wanaofanya mitihani ya kidato cha pili katika shule ya Mchangamdogo Pemba.

Aliwataka wanafunzi kutoa taarifa kama watabaini baadhi ya mambo ambayo sio ya kawaida ikiwemo vitendo vya udanganyifu wa mitihani.

Alisema wizara imejipanga kuhakikisha kwamba matukio ya vitendo vya udanganyifu yanadhibitiwa na kuepuka kuitia hasara serikali.

"Nimetembelea baadhi ya shule na wanafunzi wanaofanya mitihani kidato cha pili na nimeridhika na mitihani hii,"alisema.

Aidha, aliwataka walimu wanaosimamia mitihani hiyo kufuata maadili ya kazi zao ili kuhakikisha mitihani hiyo inamalizika bila ya kuwepo kwa vitendo vya udanganyifu ambavyo vitawahusisha walimu.

Alisema mitihani ya kidato cha pili ambayo ilihairishwa Desemba mwaka jana kutokana na kuwepo kwa udanganyifu imeisababishia hasara kubwa wizara yake.

Alieleza kuwa bado wizara yake inaendelea na uchunguzi ili kuweza kuwabaini waliohusika na udanganyifu huo ambao ni kinyume na maadili ya kazi ya ualimu.

Wanafunzi wa kidato cha pili Unguja na Pemba wanaendelea na mitihani yao ya taifa baada ya wizara ya elimu kutoa mitihani mipya baada ya kufuta ile ya awali kutokana na kuvuja.

Nipashe
MWANGA WA JAMII


BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JANUARI 19, 2019



## ISHA ANAPOTAMBIA MAADILI

Soma UK.14




# TAMU NA MACHUNGU YA HAMZA KALALA

## BASI SAWA



## Amini yeye mdogomdogo tu

AMIN Mwinyimkuu amesema licha ya kurudi katika gemu kwa mafanikio, lakini amekuwa na tahadhari kulinda soko lake la muziki.

"Lengo langu ni kufanya mapinduzi katika kazi zangu, ni lazima kuwa makini na kufanya mambo kwa tahadhari wakati unapotoa singo," amesema Amin.

Amesema yeye ni msanii mkubwa ambaye ana mashabiki wengi, hivyo kutoa nyimbo mfululizo bila kuangalia soko inaweza kumuondoa katika njia.



## Phantom Musica waipua wimbo 'Sekidobwa'

BENDI ya muziki wa dansi ya Phantom Musica International imekamilisha kurekodi wimbo wao mpya unaojulikana kwa jina 'Sekidobwa', ambao tayari umeanza kusikika katika vituo mbalimbali vya redio nchini.

Akizungumzia na BT, kiongozi wa bendi hiyo Abdulfareed Hussein, alisema kurekodiwa kwa 'Sekidobwa' ni hatua ya kutimiza ahadi waliyoiweka mwishoni mwa mwaka 2018.

Alisema, awali walizungumzia ujio wa kibao hicho kipya kama kuwatayarisha wadau wa muziki wa dansi kukaa mkao wa kula kusikiliza ni kwa namna gani wana Phantom Musica wanaunza mwaka mpya wa 2019.

"Tuliweka hadharani kila hatua ya nini tunakuja nacho ifikapo mwanzoni mwa mwaka huu na sasa tumetimiza ahadi na hii 'Sekidobwa'".



## Isha anapotambia maadili

MWIMBAJI nyota wa muziki wa taarab nchini, Isha Mashauzi amesema wasanii wa fani hiyo wanaendelea kuwa maarufu kutokana na tabia zao za kukaa mbali na kashfa.

Akizungumza na BT, Isha amesema muziki wa taarab utaendelea kuwepo baada ya watu kuona ni muziki pekee unaojali maadili mema na kufanya mashabiki na wasanii kuheshimiana.


"Wasanii wa muziki wa taarab hawategemei kiki kwenye kazi zao, wanaheshimu kila mtu na hasa mashabiki na ndio maana umaarufu wetu unabaki palepale," amesema Mashauzi.

## INSTA-TWITTER





**Usijisifu** Una Mbio, Msifu na Anae Kukimbiza-**Linnah.**



**Muda** mwingine najiona bonge, ila kuna muda najiona kipotabo-**Rose Ndauka.**



## Nacha awatambia 'Hadithi' kizamani

NI ubunifu mwingine imetikisa Bongo Fleva, baada ya rapa Nacha kutoa singo mpya ambayo imeonyesha jinsi gani tasnia ya muziki inazidi kuwa juu.

Nacha alitambulisha video ya wimbo huo unaoitwa 'Hadithi' juzi na kupokelewa vizuri na mashabiki wa muziki.

Kwenye 'Hadithi' utaona kazi nzuri iliyofanywa na prodyuza Kitonzo, huku video ikiongozwa vyema na Deo Abel.

**UNASEMAAA...**

## Suma Lee aibuka na dua nzito makaburini

MKONGWE wa muziki ambaye kwa sasa amegeukia mafundisho ya dini, Suma Lee, amewashukuru watu wote waliokwenda kumfariji mwanamuziki Ali Kiba ambaye amefiwa na baba yake mzazi.

Akizungumza mbele wa Waziri wa Maliasili na Utalii, Hamis Kigangwalla, amesema msiba huo umewahusa wengi na kwenda kumzika mzee Kiba ni jambo linalowapa faraja.

Aidha Suma Lee ameomba dua zito kwa familia hiyo baada ya kumaliza mazishi katika makaburi ya kisutu jijini Dar es Salaam.



**BODA 2 BODA**

## 'Mbele Kwa Mbele' dunia nyingine



UNAWEZA kusema amebadilika! Ndivyo wimbo mpya wa Nay wa Mitego, unavyomtafasiri na kuonyesha jinsi gani amebadilika katika uimbaji wake.

Wimbo huo 'Mbele Kwa Mbele' umemleta rapa huyo mwenye utata katika dunia mpya ya muziki baada ya kibao hicho kupigwa katika mtindo tofauti na ule uliozoeleka kwa mwanamuziki huyo.

Vionjo vitamu vinapatikana katika ngoma hiyo ilimendaliwa na Hanscana huku rapa Roma Mkatoliki na mtayarishaji wa muziki T Touch, wakionekana kwa mbali.

Kwa ujumla ngoma ya 'Mbele Kwa Mbele' imemtambulisha Nay Wa Mitego mpya na baadhi ya mashabiki wake wampempa sifa kwa muonekano wake huo wa sasa.




@burudanitele

>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow

**INSTA-TWITTER**



Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Jamani** kama kuna single mother humu ndani, jueni tu kwamba nawapenda jamani, na namuomba Mungu azidi kuwapa nguvu kulea watoto wenu-**Zari.**



**Wanaotafuta** picha zao za miaka 10 iliyopita kama huzioni nipe mimi hiyo kazi nitakuletea popote pale ulipo. We niambie tu 2009 ulikuwa wapi-**Billnas.**



**Mwenzenu** kuna mtu nampenda, otea nani-**Gigy Money.**

# Kuumbe!

# HAMZA KALALA

## Alianzisha Vijana Jazz Band bila malipo



Na Adam Fungamwango

VIJANA Jazz Band ni moja kati ya bendi kongwe hapa nchini. Ilianzishwa mwaka 1970 jijini Dar es Salaam na baadhi ya wanamuziki waliokuwa wakifanya kazi kwa kujitolea.

Bendi hiyo ilinzishwa na Umoja wa Vijana Tanzania.

Hamza Kalala, mmoja wa wanamuziki wakongwe na maarufu kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki alikuwa mmoja wa waanzilishi wa bendi hiyo.

Wengine ni Issa Chikupele, Mohamed Mtono, Abdallah Kwesa, Hassan Dalali, Athumani Kilingo na wengineo.

Kwa mujibu wa maelezo ya mwanzilishi mwenyewe mtunzi, mpiga solo na mwimbaji Comandoo Hamza Kalala ni kwamba awali Umoja wa Vijana ilikuwa na bendi iliyoitwa Green Guard ambayo ilikufa.

Hakuna maelezo rasmi baada ya kufa kwa bendi hiyo, lakini alipofika hapo hakuikuta zaidi ya vyombo tu.

Pia anasema hakukuwa na mpango Umoja wa Vijana wa kuifufua, wala kuianzisha bendi ya Vijana Jazz Band, lakini kuwepo kwa vyombo kulimvutia yeye na vijana wengine wanamuziki kufanya mazoezi na kupiga muziki.

Hiyo ilisababisha kuwepo kwa kundi hilo, lakini likiwa halikuwa kilipato chochote kutoka kwa viongozi wa umoja huo, zaidi ya kujitolea tu.

"Tulikuwa tunapiga muziki bure tu, ila tulikuwa tunajituma kwa sababu tulifahamu ipo siku watatuelewa tu." Anasema Kalala.

Kutokana na kufanya kazi kwa kujitolea, kulirahisisha wao kutumika au kutumiwa kwenye hafla mbalimbali za kichama na serikali, na kwa kiasi fulani kulifanya Umoja wa Vijana kuanza kuichukulia kuitambua, ingawa bado hakuna aliyekuwa akilipwa.

Kutokana kuendelea kufanya kazi nzuri, ikiwemo baadhi ya taasisi kuitumia bendi kwa ajili ya kujitangaza na kuburudisha wafanyakazi wao, hivyo wanamuziki wa bendi hiyo walianza kulipwa na taasisi hizo, hivyo Umoja wa Vijana nao ulianza kuona kuna faida mbele, hivyo ulianza kuwalipa wanamuziki posho ya Sh. 50/=.

**KUPELEKWA JKT**

Kalala anasema siku moja Naibu Katibu Mkuu wa Vijana wakati huo Andrew Shija, aliona vijana wamezagaa kwenye Makao Makuu na kuuliza walikuwa ni akina nani.

Alipoambiwa kuwa ni wanamuziki wa bendi, alipowatazama aliona kama watu wasio na nidhamu hivi, hivyo aliagizwa wamepekwe Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), hivyo Hamza na wenzake walikwenda kupiga kwata kwa miezi sita.

Ikumbukwe kuwa wakati wote huo, mwanamuziki maarufu wa bendi hiyo Hemed Maneti alikuwa bado hajajiunga na bendi hiyo.

**KUTAMBULIWA VIJANA BAND**

Baada ya kuhitimu mwaka 1973, waliendelea na muziki, mwaka mmoja baadaye walikwenda mjini Zanzibar kwa ajili ya maombolezo na mwaka mmoja baada ya kifo cha Makamu wa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, mheshimiwa Sheikh Abeid Amaan Karume.

Kalala anasema kuwa nyimbo walizoimba za maombolezo ziliwafurahisha na kuwaliza wengi kiasi cha Makamu wa Rais wa wakati huo Rashid Mfaume Kawawa kuuliza ni bendi gani ile.

Alipojibiwa kuwa ni bendi ya Umoja wa Vijana na ni wanamuziki wanaojitolea tu hawalipwi zaidi ya posho tu ya Sh. 50, aliuliza kwa nini wasitumike sasa kwenye shughuli kama zile za kisiasa, kiserikali na kichama, kwani pamoja na kuwepo kwa gazeti, lakini uwepo wa bendi ni mzuri zaidi kwani nyimbo zikitungwa na kurekodiwa kukaa vichwani mwa watu zaidi na kueleweka zaidi kwa jamii.

Ushauri wa kiongozi siku zote huwa ni kama amri. Rasmi sasa bendi ya Vijana Jazz ilitambulika rasmi na kumilikiwa na Umoja wa Vijana wa Tanzania, ikiwa kama ni moja ya mali za umoja huo.

Hapo ndipo wanamuziki walipoanza kulipwa mishahara kutoka Makao Makuu na walianzia na mshahara wa Sh. 150/=

Hapo ndipo bendi hiyo ilipoanza kuonyesha cheche zake na kuwa moja ya bendi kubwa na tishio kwa bendi zingine Tanzania. Nyimbo kama 'Niliruka Ukuta', 'Operesheni Maduka', 'Masido', 'Shoga', 'Wifi zangu mna Mambo', 'Aza Umeniumbua', na nyingine nyingi.

Bendi hiyo imepitiwa na wanamuziki wengi mahiri kama Maneti, Kida Waziri, Adam Bakari, Eddy Sheggy, Benovilla Antony, John Kitime, Suleiman Mbwembwe, Maximillian Bushoke, Cosmas Thobias Chidumule, Shaaban Yohana 'Wanted', na wengine wengi kwa nyakati tofauti.

# BENDI ZA MAAFANDE ZILIZOTAMBA URAIANI

Na Adam Fungamwango

MWALIMU Julius Kambarage Nyerere alianzisha sera ya Makampuni, Mashirika ya Umma, Wizara, na hata Majeshi ya Ulinzi na Usalama kuwa na vikundi vya Michezo na Utamaduni.

Taifa lolote lisilokuwa na utamaduni na taifa mfu. Hayo yalikuwa ni maneno yake.

Hapo ndipo zilizopoanzishwa bendi nyingi nchini Tanzania zilizomilikiwa na Mashirika ya Umma na Kamapuni.

Mfano ni Bima Lee ikimilikiwa na Shirika na Bima ya Taifa, UDA Jazz, ikimilikiwa na Shirika la Usafirishaji Dar es Salaam, kwa sasa UDAT maarufu kama Mwendokasi, National Panasonic cha Kampuni ya kutengeneza betri na nyingine nyingi.

Kwenye majeshi nako kulianzishwa bendi ambazo baadhi zilivuma mno na kuteka hisia za mashabiki wa muziki wa dansi nchini.

Zilikuwa za majeshi, lakini zilikuwa na mashabiki wengi hadi uraiani kutokana na kuwa na nyimbo zilizovutia.

Hizi ni baadhi ya bendi hizo.

**Mwenge Jazz Band**

Unaweza ukasema kuwa hii ndiyo bendi mama ya Majeshi yote nchini.

Ni bendi maarufu zaidi nchini na iliyokuwa na wapenzi wengi kuliko bendi nyingine ya jeshi.

Mwenge Jazz inayomilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ilikusanya wanamuziki mahiri kutoka bendi mbalimbali nchini na kuifanya moja ya bendi ya kuogopwa na bendi zingine za uraiani. Wanamuziki kama Mohamed Salum 'Gotagota', Mgoro Mohamed, Luza Elias, Msafiri Haroub, Mhina Panduka 'Toto Tundu', Shomari Ally, Benovilla Antony na wengineo wengi waliifanya bendi hiyo kuwa moto wa kuotea mbali.

Nyimbo zilizoiweka bendi hiyo kupendwa zaidi uraiani ni 'Rehema', 'Pole Baba James', 'Kupatwa kwa Mwezi', 'Tofali la Barafu', 'Chenga Bin Utoe', na nyingine nyingi. Bendi hii bado ipo ingawa haina makali kama yale ya zamani. Inaongozwa na Shukuru Majaliwa anayefanana kiwajihi na sauti na mwanamuziki wa zamani wa Msondo Ngoma, Tx Moshi William.

**Kimulimuli Jazz**

Bendi hii ilijulikana zaidi kwa jina la Kimulimuli. Lakini jina halisi ni JKT Mafinga, ikiwa na makao makuu yake Mafinga mkoani Iringa.

Ilikuwa inamilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa huko Mafinga.

Jina la Kimulimuli lilipatikana kutokana na kupata vyombo vipya ambayo vilikuwa vinawaka taa na kuzima, hivyo mashabiki wakaipachika jina hilo.

Iliundwa kutokana na mabaki ya wanamuziki wa JKT Kimbunga Stereo, ambao walipelekwa huko kuunda kile kilichoonekana kama kuunda kikosi cha pili kutokana na kuwa wengi sana. Hata hivyo ikawa ndiyo bendi bora zaidi ya JKT kuliko nyingine yoyote kwenye historia ya muziki wa Tanzania.

Pia ikawa inashika nafasi ya pili nyuma ya Mwenge Jazz kwa ubora kwa bendi za majeshi nchini.

Ubora wa bendi hiyo ulichagizwa na kuwepo kwa mwanamuziki Zahir Ally Zorro ambaye aliipaisha na kiasi cha kuifunika bendi mama ya Kimbunga Stereo.

Nyimbo kama 'Makiwa', 'Cecilia', 'Kabwe', 'Photo Album', 'Christina', 'Tikisa' na nyingine, zilitikisa anga la muziki wa Tanzania.

**JKT Kimbunga Stereo**

Bendi hii ilimilikuwa na Jeshi la Kujenga Taifa Mgulani jijini Dar es Salaam. Ilikuwa moja ya bendi bora nchini za majeshi nchini.

Na ilikuwa kwenye kilele cha mafanikio ilipokuwa chini ya Kapteni John Simon (marehemu), Muharami Said (marehemu) ambaye baadaye alikwenda DDC Mlimani Park.

Ilitamba sana ni nyimbo za 'Utukufu wa Chama', 'Majambazi', 'Cheza Rhumba Kimbunga', 'Chakula Cha Shida', 'Ushirikina' na nyingine nyingi.

**CTU Les Mwenge Jazz**

Hii ni bendi iliyomilikiwa na Jeshi la Wananchi Tanzania, lakini ikiwa na maskani yake jijini Arusha.

Ilikusanya baadhi ya wanamuziki na kuunda bendi iliyoondokea kuwa tishio, ingawa kwa muda mfupi tu. Ilikuwa na baadhi ya wanamuziki nyota kama mzee Ahmed Manyema (marehemu), Harilla Tongolanga (marehemu) na wengineo. Ilitamba na kupata mashabiki wengi kutokana na kibao kama 'Kila Munu Ave na Kwao' ule wa kwanza kabisa.

**Magereza Jazz Band**

Ni moja kati ya bendi kongwe za majeshi nchini. Inamilikiwa na Jeshi la Magereza. Bado ipo, ingawa haivumi kama ilivyokuwa wakati ule.

Imepitia awamu nyingi, lakini awamu inayokumbukwa zaidi ni ile iliyokuwa na kina Abel Bathazar (marehemu), Hassan Kunyata, Nana Njige (marehemu), Makoye Kwelukilwa na Chibanda Soni ikiwa na mtindo wa 'Mkote Ngoma'.

Ilivuma mno na kupendwa na raia kutokana na vibao vya kama 'Edina', 'Ashura' na nyingine nyingi.



Mwenge Jazz

# Vijimambo




1. Utalii mubashara. Ila ni hatari kwa uhai - Shirima, Nanenane Morogoro.
2. Wewe unamjua huyo jamaa au? - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
3. Akiinuka hapa, napotea kama umeme Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
4. Chezea huyo huyo simba wa sarakasi, usijaribu simba wa Mikumi - Moussa Benali, Zenji.
5. Waarabu nishawafunga, sasa wananichua misuri nimfunge Vita wa Zamani - Moussa Beneali, Zenji.
6. Natamani nimuone atakavyokuwa baada ya simba kusimama. Balaa! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Oya, mbona unanizingua bwana, niache nilale - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Wewe kaache, kanajua nimezimia - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
9. Simba kitu gani bwana, mie ndio kidume - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
10. We si unajifanya mjanja ukiwa porini, sasa onyesha ujabali wako hapa mjini - Beatrice Binala, Mbeya.
11. Leo umepatikana, huna ujanja - Joseph Jalika, Matombo.
12. Hahahaa, kweli naamini. Hata Zanzibar maeneo ya Malindi simba kanyweshwa chai - 0718 409 030.
13. Nipapase vizuri, nisije nikakugeuzia kibao kwani umenona kweli - Berkmans Makumbuli, Mtwara
14. Kaka usione katulia huyo, akikasirika umekwisha - George, Upanga.
15. Operesheni nyingine hizi! Samahani - 0715 555 233.
16. Dokta taratibu basi, mguu wenye tatizo ni huo mwengine - Mfaume Mbungi, Mshindo Iringa.
17. We rafiki, mbona kamwiba kenyewe kadogo hivyo upo hoi! - 0755 083 120
18. Huyo mwarabu ndio maana aliliwa na simba kwa Mchina. Unawezaje kumchezea simba hivyo? - Dinna Gumbo, DSM.
19. Utalii wa aina hiyo fanyeni na simba wenu wa huko huko, sio hawa wetu, mtajuta - Pili Chengu, Matipwili Bagamoyo.
20. Nasikia raaaha, ninyooshe hivyo hivyo maana kasungura nilikokambiza kalikua kasumbufu! - Pili Chengu, Bagamoyo.
21. Oya, mbona unanizingua bwana, niache nilale - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
22. We si unajifanya mjanja ukiwa porini, sasa onyesha ujabali wako hapa mjini - Beatrice Binala, Mbeya.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Waarabu nishawafunga, sasa wananichua misuri nimfunge Vita wa Zamnia - Moussa Beneali, Zenji.**

**PICHA MPYA**



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Penzi haligawanyiki kinasaba

**Na Adam Fungamwango**

KISA kilichomo kwenye filamu ya D.N.A kinaonyesha kuwa penzi ni kitu cha ajabu sana. Penzi siku zote huwa halilazimishwi, bali hutokana na ridhaa ya mtu mwenyewe.

Anayependa huweza hata kutoka kwenye nyumba ya kifalme na kwenda kuishi kwenye tembe la wafugaji.

Yoyote yule mwenye uwezo wa kipesa au cheo, hawezi kumlazimisha mtu ampende kutokana na kuwa na vitu hivyo, bila ya mwenyewe kuridhia.

Filamu hii imechezwa na mwanamuziki Banana Zorro, Jacob Steven JB, Suleiman Barafu, Sabrina Rupia 'Cathy' na wengineo.

Watu waliojulikana wavunja nyumba ya daktari bingwa, Banana na kumteka mtoto wake. Haijulikani kwa nini.

Siku chache baadaye anaokota barua chini ya mlango wa nyumba yake. Inamtaka kubadili majibu ya vipimo vya mmoja wa watu waliokuja kupima vinasaba D.N.A kwenye hospitali yake. Anatakiwa aandike kuwa vinasaba vya mtoto havifanani kabisa na vya mtu anayetajwa kuwa ni baba yake mzazi.

Dk. Banana anaonywa kama asipotekeleza, basi ajiandae kupokea kichwa cha mtoto wake.

Upande wa shilingi kuna mtu mmoja anaitwa Barafu. Huyu ni mfanyabiashara mwenye uwezo mkubwa. Siri ya utajiri au biashara zake haijulikani. Katika pitapita zake anakutana na msichana Cathy.

Wanasalimiana na kuchangamkiana. Wanajuana sana. Walisoma wote shule ya msingi hadi sekondari. Baada ya hadithi ndefu za zamani, wanaulizana kuhusu maisha ya sasa. Cathy anamwambia mwenzake kuwa ameshaolewa. Jibu hilo halikumpendeza Barafu. Tayari alionekana kumpenda Cathy. Kuna siku anamualika kwenye chakula cha mchana na kumwambia kuwa anataka amuache mumewe aolewe na yeye. Cathy anakataa na kumcharukia Barafu. Kwa hasira Barafu anatengeneza mpango wa kumfanya JB mumewe Cathy amuache mkewe. Anaandika waraka kwenda na JB kumwambia kuwa mkewe si muaminifu na hata mtoto waliyenaye si wa kwake, bali ni wake Barafu. Akamaliza na kumpachikia picha walizopiga wakiwa sekondari na kwenye semina.

JB anaamua kufanya uhakiki kwenye vinasaba, hivyo kazi hiyo alipewa Dk. Banana.

Ukweli ulipindishwa. Ikaonekana mtoto si wa JB. Kabla hajaamua kufanya lolote, askari polisi na wananchi wema, wanamuokoa mtoto kutoka kwenye mikono ya watekaji na kumrudisha kwa Banana.

Naye anaamua kuuweka ukweli wote wazi kuwa mtoto ni wa JB, ila alitoa majibu ya awali ya uongo kutokana na kumuokoa mtoto wake aliyekuwa ametekwa.

**Simu 0716 350534.**
**afungamwango@gmail.com**



# WATOTO WA KUPANDIKIZA

## Kardashian, Kanye West kupata mwingine

**LOS ANGELES,** Marekani

KIM Kardashian West amethibitisha kwamba yeye na mume wake, Kanye West wanatarajia kupata mtoto wa nne.

Katika kipindi cha televisheni cha 'Watch What Happens Live with Andy Cohen,' Kardashian pia amebainisha kwamba mtoto wanayemtarajia ni wa kiume.

Aliongeza kwamba mtoto huyo atawasili mapema hivi karibuni.

Mtandao wa TMZ umeripoti kuwa wanandoa hao wanapata mtoto huyo wa nne kwa kupandikiza mbegu za Kanye kwa mwanamke mwingine, kama walivyofanya kwa mtoto wao wa tatu, Chicago, ambaye alizaliwa mwaka jana.

Katika kipindi hicho Kardashian alisema mtoto huyo aliyepandikizwa kwa mwanamke mwingine kwa sababu yeye kwa sasa haruhusiwi kubeba ujauzito.

Cohen ndiye aliyemuuza Kardashian "Mnatarajia kupata mtoto mwingine? Na mwanamitindo huyo na muongozaji wa kipindi cha maisha halisi kwenye televisheni, alijibu: "Ndio tunatarajia."

Kardashian West, ambaye kwenye shoo ya televisheni hiyo alikuwa pamoja na wadogo zake, Kourtney na Khloe, alisema mtoto huyo atakuwa wa kiume na atawasili hivi karibuni.

Wadogo zake hao walionekana kushangazwa na taarifa hizo na Kardashian West mwenye umri wa miaka 38, alisema: "Ndio. Nililewa mno wakati wa sikukuu ya Krismas na niliwaambia watu.

"Lakini sikumbuki ni nani nilimuambia, kwa sababu sijawahi kulewa vile."

Habari za ujio wa mtoto huyo zimekuja baada ya uvumi kuenea kwamba familia hiyo inataka kuwa na watoto wengi.

Wanandoa hao tayari wana watoto watatu ambao ni binti yao North mwenye umri wa miaka mitano, Saint wa kiume mwenye miaka mitatu na Chicago ambaye ni wa kike ambaye alizaliwa Januari mwaka jana.

Kim amewahi kunukuliwa akisema kuwa yeye na mume wake Kanye West wanataka kuwa na watoto angalau saba, na wataendelea kuzaa kila inapohitajika.

Hata hivyo, watoto watakaozaliwa hivi sasa watakuwa wa kupandikiza kwa sababu Kim kwa sasa haruhusiwi kubeba ujauzito baada ya kupata matatizo kwenye mimba zake mbili za kwanza.

# Wizkid kuna rafiki au mnafiki



ALIYEKUWA rafiki wa mwanamuziki Wizkid, ameibuka na kudai kwamba yeye ana fedha za kutosha kuliko staa huyo.

Akitumia mtandao wa Instagram, Sarumi ambaye huko nyuma alikuwa rafiki mkubwa wa nyota huyo aliweka picha ambayo inaonesha wakiwa wawili wakati wa enzi hizo na kuandika ujumbe unaosema yeye ni tajiri kuliko Wizkid.

Kulingana na ujumbe huo baadhi ya mashabiki wa Wizkid walikuja juu na kudai Sarumi anatumia picha hiyo kutaka umaarufu.



## Kylie Jenner hata yai kwake stori

KILA anachokifanya staa ni habari! Ndivyo mwanamitindo na mwanafamilia ya Kardashian, Kylie Jenner, alivyojikuta akipata wafuasi wengi kwa kuweka posti ya kawaida tu.

Kylie alishangazwa na kitendo cha kupata watu milioni 25.1 kwa kuweka picha ya yai tu katika akaunti yake ya Twitter.

Posti hiyo ya picha ya yai aliiweka Januari 4, mwaka huu 2019, ilitanguliwa na ile ya mtoto wake ambayo ilitembelewa na watu milioni 18.2.

## Christabel kumbe kuibiwa kubaya

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Christabel Egbenya, amemshukuru Mungu kwa kumuona mwizi aliyevamia duka miaka mitatu iliyopita.

Christabel aligundua mtu aliyeiba vitu ndani ya duka lake kupitia mtandaoni baada ya kuona video ya mtu akipigwa na kuingizwa kituo cha polisi na alipomuangalia aligundua mtu huyo alitaka kumuibia mwaka 2017,

Akishiriki video hiyo, staa huyo alieleza kwamba mwizi huyo alikwenda dukani kwake alijaribu kuiba lakini alishindwa baada ya kuonekana kupitia kamera za ulinzi.





## Harusi ya Baiber kutoa funzo Marekani

HARUSI ya kufa mtu! Pengine unaweza kusema hivyo baada ya maandalizi ya aina yake ya harusi ya Justin Baiber na mchumba wake Hailey Baldwin kukamilika.

Kwa mujibu wa mtandao wa Pagesix, familia za pande mbili zimekamilisha taratibu zote ikiwamo kadi za mwaliko zimesambazwa na maandalizi mengine ya upambaji na Dj wa Baiber mwenyewe, Dj Tay James ndiye atahusika kutoa burudani.

Harusi hiyo inakuja licha ya Baiber na Hailey kufunga ndoa ya kisheria tangu mwezi Septemba mwaka jana na tayari wameshaanza maisha yao ya ndoa,

## Davido anapotingisha wazungu Uingereza

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Davido, yupo nchini Uingereza kuandaa shoo yake ya nguvu itakayofanyika hivi karibuni.

Akiwa jijini London, Dabido, ameonekana akiwa ametinga mavazi ya bei mbaya akikata mitaa na kuwafanya mashabiki wake kupagawa.

Tamasha hilo ambalo litafanyika katika ukumbi wa O2 arena limekuwa gumzo katika mitandao ya kijamii na picha za msanii huyo akiwa nchini humo zikisambaa kwa kasi.



SAFU



Na John Juma
0716217615

Mionzi ya Sheria

# 'Kuwaadhibu papo kwa papo wasio na leseni ni kuwaonea'

WIKI hii Waziri wa Mambo wa Ndani, Kangi Lugola, amewaondoa kazini makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Temeke, Ilala na Arusha kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupuuza maagizo yake na kumkejeli.

Aidha, uonevu kwa madereva wa boda boda umetajwa kuwa sababu nyingine, kuchukua rushwa, kusindikiza wahalifu na kujiona miungu watu , badala ya kuwahudumia wananchi.

Hilo ni jema, ila suala jingine ambalo ingefaa Waziri Lugola na Makanda wa Mikoa wakiwamo wa Usalama Barabarani walione ni malalamiko ya kuwatoza watu faini kinyume cha sheria kisa wameshindwa kuonyesha leseni mara moja kwa polisi anapowataka kufanya hivyo.

Nianze kwa kusema pengine wewe ni raia au mmiliki wa chombo cha usafiri na siku moja ukaona malumbano au ukahusika, polisi anataka leseni na dereva anajibu kuwa hajatembea nayo kwa wakati huo na anamtaka aweke gari pembeni.

Swali ni hili, hivi ni kosa kwa dereva, anaposimamishwa na trafiki, kushindwa kutoa leseni ndani ya muda unaotakiwa kutozwa faina papo hapo? Kusimamishwa na trafiki barabarani na ukawa huna leseni mfukoni kwa muda huo si kosa. Mwambie huyo polisi kuwa kutokutembea na leseni mfukono hilo si kosa. Sheria inaagiza kutembea na leseni unapoendesha vyombo vya moto, lakini pia haisemi kuwa utakapokuwa hauna leseni pale polisi anatakapoihitaji basi ni kosa la jinai na uadhibiwe.

MWONGOZO KISHERIA

Inayozungumziwa hapa ni Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168. Wapo watu wameandikiwa faini kisa wameombwa leseni wakasema hawana, au wakajibu kuwa wamezisahau majumbani. Hawa waliotozwa faini katika mazingira kama haya wameonewa. Na wanastahili kurudishiwa fedha walizotoa haraka.

Ni kweli kifungu cha 77 cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168 kinamtaka kila mwendesha chombo cha moto kutembea na leseni barabarani.Aidha , askari anayo mamlaka kumsimamisha mwendesha chombo cha moto na kumtaka aonyeshe leseni yake, lakini si kweli hata kidogo kuwa mwendesha chombo cha moto asipoonyesha leseni kwa wakati huo basi tayari ametenda kosa. Si sahihi wala si kweli.

Kifungu cha 77(1) cha Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 kinasema kuwa mtu hatatiwa hatiani, kwa maana ya kulipa faini au kuandikiwa kosa au kuadhibiwa na chombo chochote ikiwamo mahakama, kwasababu tu hakubeba, au hakutoa wala kuonyesha leseni pale alipotakiwa kufanya hivyo.

Aidha, kinaongeza kuwa, isipokuwa ana siku tatu za kutoa au kuonyesha leseni hiyo toka siku hiyo aliposimamishwa na mamlaka na kuhojiwa au kutakiwa kuonyesha.

Hivyo basi, tafsiri iko wazi kuwa unaposimamishwa, ukaombwa kuonyesha leseni, ukawa huna kwa muda huo, unazo siku tatu mbele za kutakiwa kuleta na kumwonyesha trafiki au mamlaka nyingine zilizoulizia uhalali wa nyaraka hizo. Anachotakiwa kufanya askari si kukuandikia kosa, la hasha, bali ni kukutaka umuonyeshe leseni hiyo ndani ya siku tatu tokea dakika au wakati huo alipokuuliza. Ukishindwa kufanya hivyo ndani ya siku hizo hapo ndipo linaweza kuwa kosa.

Watu wasionewe. Wapo askari wengine pia hawajui hizi sheria. Ni wakati wa madereva kuwaelimisha. Hakuna kudhani kuwa askari anakuonea kumbe naye hajui. Kwahiyo kazi unayo wewe kuhakikisha unamweleza huyo askari kuhusu kifungu hiki na namna kinavyotaka. Wewe ndiye mtetezi wa kwanza wa haki yako kabla ya kutetewa na mwingine.

Na kama itatokea ukaandikiwa adhabu kwa lazima kwa kitu kama hiki, basi unayo haki ya kukataa kulipa na kuomba kufikishwa mahakamani ili sheria ikatafsiriwe.

Mwambie "sitalipa nataka sheria ikatafsiriwe mahakamani".

Kukataa kulipa si kosa au ukorofi na hivyo huna haja ya kuhofu.Kukataa kulipa ni haki katika haki ulizonazo ukihisi umeonewa.

Na kama umeshalipa au ulilipa huko nyuma katika mazingira ya jambo kama hili na unao ushahidi basi unayo haki ya kudai hela uliyolipa. Unaweza kuidai huko ulikotozwa au mahakamani.

Sheria imetoa ahueni hii ikizingatia mazingira ya ubinadamu. Huwezi kila unapoamka asubuhi ukakumbuka leseni. Huwezi kila unapokuwa na safari ukakumbuka leseni. Safari nyingine ni za ghafla na za kushtua, mfano kuitiwa msiba,ugonjwa,matatizo kazini,bila kusahau msongo/stress za ada na kodi. Atapata wapi muda wa kukumbuka leseni mtu huyu.

Mwingine amebadilisha nguo na hivyo leseni kubaki kwenye nguo iliyovuliwa, mwingine amebadilisha gari na hivyo leseni kubaki kwenye gari jingine.

Na mazingira mengine kama hayo. Zote hizi ni dharura za kibinadamu zilizowafanya watunga sheria kuweka muda wa siku tatu kwa ajili ya kutoa au kuonesha leseni.

Ni wito, watu wabadilike, madereva na askari wasimamia usalama barabarani. Dereva asiwe mkorofi, kadhalika askari asimwonee dereva au abiria wanapozungumzia suala la leseni.



Reubeni Lumbagala

Kalamu ya Mwalimu

# Jinsi ufaulu unavyoongezeka, maslahi ya walimu yaimarike

WALIMU ni nyenzo muhimu katika kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wenye matokeo chanya kwa wanafunzi. Wanataaluma hawa ndiyo wapishi wa kuwaandaa vyema wanafunzi kupata maarifa, ujuzi, stadi na mbinu mbalimbali za kitaaluma na kimaisha wawapo shuleni.

Hawa ndiyo hufanya kazi kubwa katika kuhakikisha wanafunzi wanapata kile ambacho kinatarajiwa kupatikana shuleni ili kuwapa hatma na mwelekeo bora maishani.

Kutokana na kazi kubwa inayofanywa na walimu nchini, ufaulu wa wanafunzi unaongezeka mwaka hadi mwaka na kuleta faraja kubwa hasa kwa wazazi na walezi wenye watoto wanaosoma katika shule za msingi na sekondari.

Pia, kazi nzuri inayofanyanywa na walimu shuleni imeongezea serikali imani kubwa kwa na utekelezaji wa majukumu waliyopewa ingawa si wote wanaowajibika ipasavyo.

Walimu wanajitahidi kufundisha kikamilifu ili kumaliza mada kwa wakati na kufanya marudio na mazoezi ya kutosha ili kuwaandaa vyema wanafunzi kwa mitihani ya baadaye.

Baadhi ya shule wamejiongezea muda wa kufundisha hadi saa 11 jioni ili kuhakikisha walimu na wanafunzi wanapata wakati wa kutosha wa kufundisha na kujifunza ili kupata matokeo bora.

Walimu pia wamekuwa wakijitolea kufundisha siku za mwisho wa juma na kutoa mazoezi na majaribio mwngi kwa wanafunzi ili kuwaandaa vyema kukabilia na mitihani iliyo mbele yao.

Haya yote yanafanywa na walimu wenye mioyo ya kizalendo katika kuchangia ukuaji wa taaluma na ufaulu wa wanafunzi.

Matokeo ya mtihani wa upimaji darasa la nne mwaka 2017 ulionyesha ufaulu kufikia asilimia 93.13 lakini mwaka 2018 ulipanda kwa asilimia 0.03 na kufikisha asilimia 93.16. Mwaka 2016, ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba ulikuwa ni asilimia 70.36. Mwaka 2017 ufaulu uliongezeka kwa asilimia 2.40 na kufikia asilimia 72.76.

Mwaka 2018, ufaulu wa darasa la saba ulipanda tena kwa asilimia 4.96 na kufanya ufaulu kufikia asilimia 77.72. Mwaka 2017, ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha pili ulikuwa ni asilimia 89.32 lakini mwaka 2018 uliongezeka kwa asilimia 0.36 na kufikia asilimia 89.68.

Hivyo basi, mafaniko haya ni mwendelezo wa kazi nzuri inayofanywa na walimu katika kujituma kuwafundisha vyema wanafunzi hao.

Wakati wazazi, walezi, serikali pamoja na wananchi wote kwa ujumla wakifurahia matokeo mazuri yanayosababisha kuongezeka kwa wastani wa ufaulu kitaifa, kazi inayofanywa na walimu inapaswa kutazamwa na kuthaminiwa kwa jicho la kipekee.

Eneo muhimu na la kipekee ni maslahi na stahili za walimu. Serikali imefanya kazi kubwa katika kushughulikia madai mbalimbali ya walimu lakini bado zipo changamoto nyingi zinazowakabili.

Mishahara ya walimu bado ni midogo kulinganisha na kazi kubwa wanayoifanya katika kulitumikia taifa hili. Kutokana na serikali kukamilisha zoezi la uhakiki wa watumishi, mwaka 2019 serikali iangalie namna bora ya kuwaongezea walimu nyongeza ya mishahara ambayo itasaidia kuwapunguzia walimu makali ya maisha.

Pia suala la kuwapandisha walimu madaraja katika bajeti ya mwaka 2019/2020 lipewe msukumo mkubwa. Wapo walimu walioanza ajira mwaka 2013 na 2014 wenye sifa za kupandishwa madaraja lakini bado hawajapandishwa.

Kutokana na walimu hawa kutumika vya kutosha na kuongeza tija katika utumishi wao, watakapopata stahili yao itawaongezea ari kubwa ya kufundisha wanafunzi na kuchangia ufaulu.

Lipo tatizo la madai ya posho za safari. Walimu wamekuwa wakiandika barua za posho ya safari kwa wakati na kuziwasilisha katika mamlaka husika lakini kumekuwa na ucheleweshaji wa posho hizo na wakati mwingine kufikisha hadi miaka miwili bila walimu kulipwa fedha zao. Serikali kupizia Wizara ya Elimu na Tamisemi waangalie namna bora ya kumaliza tatizo hili kwani linaongeza malalamiko kwa walimu.

Sambamba na hilo, walimu pia wapewe motisha kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kutokana na uwajibikaji mzuri unaofanywa na walimu unaochangia kupanda kwa wastani wa ufaulu katika mitihani ya taifa, ni muhimu serikali kuweka utaratibu mzuri wa kuwapa walimu motisha pindi wanapofaulisha kwa kupata alama 'A' au 'B'.

Halmashauri ziweke mkakati wa kuwatambua walimu waliofaulisha vizuri wanafunzi.

Pia ruzuku mashuleni iongezeke ili Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu waweze kuwa na uwezo wa kuwapa motisha walimu kuongeza ari ya kazi kwa walimu kwani upo uhusiano wa moja kwa moja kati ya motisha na ufanisi wa kazi.

Natamani kuona mwaka 2019 uwe mwaka wa kicheko kwa walimu kwa serikali kuwapa walimu maslahi yaliyoboreshwa kwani wamejitoa kwa hali na mali kulitumikia taifa hili. Tafakari.

Reubeni Lumbagala ni mwalimu kwa taaluma kutoka Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni: 0764-666349**

NYUMBA YANGU

# Zitunze kwa usafi sofa uwe na sebule murua



Na Elizabeth Zaya

KATIKA dimba la uwanja wa nyumba leo, jicho linatua kwenye umaridadi na usafi wa sofa au kochi kubwa na la kisasa. Zama hizi watu wengi hupenda kuweka sofa sebuleni. Hivyo ni lazima kusafisha viti hivi ili kuvitunza kwa sababu ni kitu au samani muhimu ndani ya sebule.

Uzuri wa sebule ama barazani kwako, kama baadhi ya watu wanavyopita ni mpangilio wa viti, mapambo, makochi bila kusahau usafi wa kila kitu kuanzia, sakafu, ukuta, dari, madirisha na mapazia .

Makochi au sofa ni viti ambavyo hung`arisha na kuleta mvuto ndani ya nyumba kwa kuwa ni samani ya muhimu iliyoko mapokezi au resepsheni ya nyumbani kwako.

Sofa nyingine zimekuwa kijiwe cha mende ndipo yalipo mayai ya wadudu hao. Wengine wameyasahau vyakula vinavyodondoka wakati wa kula huishia humo, tangu sasa achana na tatizo hilo.

Fahamu kuwa usafi wa sofa ni muhimu kama ilivyo katika mambo mengine nyumbani, linahitaji usafi tena kwa umaridadi wa hali ya juu hususani kwa nyumba zenye familia kubwa au zenye watoto ambao pasipo kusafisha mara kwa mara zinaweza kuharibu kabisa mvuto katika nyumba.

Baadhi ya watu huwana utaratibu wa kusafisha mara kwa mara sababu mara nyingine inatokana na kutokujua kwamba makochi yanatakiwa kusafishwa ama kutokujua vitu vinavyotumika katika kusafishia na mahali pa kuvipata.



Usafi wa sebule mpangilio wa samani hasa sofa unaifanya nyumba kuwa maridadi na kuonekana kama pepo ya dunia. **PICHA: MTANDAO.**

Kutokana na kutokujua au kukosa taarifa au elimu sahihi ya namna ya kusafisha, wengi wanazifuta sofa kwa kuondoa vumbi kama kawaida au kwa kutumia maji ya kawaida na kwa kutumia vitambaa visivyofaa na mpaka kuziharibu.

Sofa zikifutwa futwa bila kusafishwa kikamilifu au kwa kutumia maji matokeo yake si mazuri kwa kuwa badala ya kung`ara huanza kuchafuka , kuchubuka na kuchakaa zaidi.

Na ikifikia katika hali hiyo, matokeo yake hata pale unapotaka kutumia njia sahihi ya kusafisha, huwa hazirudii katika mng`ao wa asili kwa sababu hulazimika kutumia nguvu kubwa na kusugua zaidi jambo ambalo husababisha kupausha rangi ama kuondoa mng`ao wa mwanzo.

**Kutokana na kutokujua au kukosa taarifa au elimu sahihi ya namna ya kusafisha, wengi wanazifuta sofa kwa kuondoa vumbi kama kawaida au kwa kutumia maji ya kawaida na kwa ...**

Kwa wale wenye sofa za vitambaa, wanatakiwa kutumia njia sahihi zaidi ya kusafishia badala ya kufuta kienyeji ili kuzitunza zisiharibike kwa sababu kitambaa ndicho kiko katika hatari zaidi ya kuharibika endapo utaratibu sahihi hautafuatwa wakati wa kusafisha.

Kuna sabuni ya maji na dawa ya kusafishia 'spray' inayotumika kusafishia sofa, ni vema ukaitafuta hiyo kwa sababu inapatikana kwa wingi.

Lakini baada ya kuipata hakikisha sofa zimepanguswa na kutolewa vumbi lote lililokuwa limeng`ang`ania kwa kutumia kifaa maalum cha kupuliza vumbi ama kwa kutumia kitambaa kisafi.

Baada ya kuhakikisha umesafisha kila kona, ndipo unatakiwa kuanza kuipulizia hiyo spray

Kwa kuzingatia ujazo katika chupa hizo maalum za maji ya kusafishia sofa unaweza kutambua utumie chupa ngapi na kwa sofa ngapi hasa kulingana na ukubwa wa tatizo japokuwa naamini moja inaweza kutosha isipokuwa uchafu wake uwe ni wa kupitiliza.

Unachopaswa kufanya ni kuhakikisha unaipulizia katika sehemu ndogondogo ili wakati huo huo uwe unafuta na kitambaa kisafi, na unatakiwa kufanya hivyo mpaka umalize.

Baada ya kumaliza kazi hiyo katika maeneo yote unaweza kuliacha kochi likauke na hapo ndipo utaanza kuona matokeo bora kwa sababu mng`ao wa rangi yake utakuwa mzuri zaidi.

Kumbuka kwamba kufanya usafi huo katika sofa hakuhitaji gharama kubwa endapo utafanya mwenyewe, isipokuwa uamue kutumia gharama kubwa kwa matakwa yako.

Na pia kadri utakavyojenga utaratibu wa kupenda kusafisha sofa mara kwa mara ndivyo hivyo gharama itazidi kuwa ndogo kwa sababu hutatumia spray nyingi kama ambavyo utasafisha zikiwa zimechafuka sana.



## MAKALA

# Hapa wafugaji, wakulima mmeshinda kwa kishindo

Na Gaudensia Mngumi

HOFU ya maelfu ya wanavijiji waliokuwa wana 'hati miliki ya kuishi kwenye mazingira magumu' imekwisha. Hawana tena wasiwasi wa kupoteza mali wala maisha, ukichukulia kuwa muda wote walikuwa na woga wa kutimuliwa, kisa wanaishi jirani na hifadhi.

Leo wamewekwa huru baada ya Rais John Mgufuli, kuagiza kusitishwa mara moja mpango wa kuviondoa vijiji 366 na vitongoji kadhaa vinavyodaiwa kuwa vimevamia maeneo ya hifadhi.

Wengi wa wanaonufaika na maagizo ya Rais ni wafugaji ambao kwa miaka kadhaa walilazimika kuhama na wanyama wao kutokana na kukosa nyanda za malisho. Wafugaji hawa walichoka kwa kutembea na mifugo yao lakini pia hawakukubalika kila walipopita kwani walihusishwa na kusababisha migogoro ya wakulima na wafugaji lakini sasa wameshinda kwa kishindo.

Aidha, pamoja na kufuta mpango wa kuondoa kwenye ramani ya Tanzania vijiji luluki, Rais anawaagiza viongozi wa wizara zote zinazohusika kwenye uhamishaji huo ikiwamo wa Ardhi na Utalii kukutana ili kubainisha na kuanza mchakato wa kurasimisha maeneo ya vijiji na vitongoji hivyo.

Watanzania hao kilichowaathiri ni kujenga na kulima karibu na hifadhi za wanyama pori ndicho chanzo cha shinikizo la kutakiwa kutimuliwa na mali zao kuteketezwa zikiwamo nyumba na mazao ya kudumu huku nyingine zikiharibiwa.

Rais Magufuli anawataka viongozi wa wizara zinazohusika na kusimamia operesheni hiyo ambazo ni pamoja na Ardhi, Kilimo, Maliasili, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kubainisha maeneo ya hifadhi za wanyamapori na misitu ambayo hayana wanyamapori au miti ili yagawiwe kwa wafugaji na wakulima ambao kwa sasa wanataabika kupata maeneo ya kufugia na kulima.



Wanyama pori na mifugo wakifurahia maeneo ya .malisho. Tatizo la ukosefu wa nyanda za malisho linahitaji kutatuliwa badala ya kuwaondoa kinguvu wafugaji na wakulima wanaoishi jirani na mifugo.
PICHA : MTANDAO



**MATESO**

Mfano Watanzania walioteseka kwa kuwa majirani wa hifadhi ambao waliishi katika mazingira magumu na yasiyo rafiki ni pamoja wakazi wa Kijiji cha Mloka wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, hawa waliuona mkono wa askari wa wanyama pori ukiwaelemea kikamilifu.

Mathalani, baadhi ya wanavijiji hao waliripoti kwa Nipashe kuwa kwa miaka kadhaa, jamaa zao waliokutwa jirani na hifadhi ya Selous walitoweka. Kwa wale waliokuwa na mifugo nayo pia haikuonekana hadi leo.

Walidai kuna baadhi waliokuwa wakivua samaki kwenye mabwawa yaliyokuwa ndani ya hifadhi hiyo nao walidaiwa kuwa walitoweka licha ya kwamba walikwenda kutafuta samaki wa kitoweo hawakurudi.

Hata hivyo, hofu ilizidi kwa kuwa vijana wa kijiji cha Mloka waliodaiwa waliingia hifadhini Selous wawe wafugaji au wavuvi baada ya kupotea na kutafutwa kwa siku kadhaa na wanavijiji, miili yao haikuwahi kuonekana.

Wanavijiji hao waliteseka na hakukuwa na mpango mkakati wa kuwarejeshea amani. Ni waziri yupi Bongo hii atasema halielewi suala la majirani wa hifadhi kuishi kwenye mazingira hatarishi?

Wanavijiji walihaha kuanzia Loliondo hadi Serengeti kuna baadhi walidai nyumba zao na maboma yalichomwa moto. Wanyama waliteswa lakini wanawake walinyanyaswa kijinsia.

Hata hivyo, chanzo cha tatizo hilo ni madai kwamba ni mipango ya kuongeza mapori lakini ukipunguza nyanda za malisho na maeneo ya ufugaji, ndiyo iliyosababisha mgogoro huo wa miaka mingi.

Nyanda za malisho ambazo ni maeneo yaliyokuwa karibu na hifadhi za wanyama pori, yalitwaliwa ili kuongeza ukubwa wa baadhi ya mbuga za wanyama na misitu lakini mifugo ikaachwa bila hatma.

Hivi kuna mkuu yeyote wa mkoa au wilaya asiye na taarifa hizi za wananchi walioweka maisha yao rehani? Baadhi ya viongozi waliamua kwa kiburi kulichukulia suala hili kuwa ni kama chemsha bongo hakuna anayeisahihisha wala kutoa alama za kushindwa ama kushinda, lakini ukweli ni kwamba wananchi hawa ni kama waliishi na kiama mikononi kwa vile waliteseka mno.

Wana vijiji hawa waliamini kuwa japo wapo duniani kuishi na kufa havitofautiani kutokana na ama kushambuliwa na kujeruhiwa na wanyama pori, kuadhibiwa kikamilifu na askari wa wanyama pori lakini pia kufukuzwa kwenye maeneo yao ya asili.

Kabla Rais hajatoa maelekezo ya kutengua mpango huo, viongozi walisahau kuwa hawa ndo waliowapigia kura ambao miongoni mwenu mwao wako madarakani. Ndiyo mawaziri na manaibu.

Je, ni kiongozi yupi wa halmashauri za miji, wilaya, jiji au manispaa zilizo karibu na hifadhi asiyezielewa shuluba wazipatazo wananchi wake? Kisa maisha jirani na hifadhi.

Yupo yeyote huko kwenye safu za vyama vya siasa anayesema hajajua hali ilivyokuwa Loliondo, Serengeti, Rufiji karibu na Selous, Sadani na hata wakazi wa Ziwa Jipe mkoani Kilimanjaro?

Rais Magufuli pia aliagiza vijiji vyote 366 vilivyoainishwa kuwapo ndani ya maeneo ya hifadhi nchini, visiondolewe katika sehemu hizo, badala yake, akawapa mwezi mmoja kwa viongozi wa wizara zote zinazohusika kubainisha maeneo ya vijiji hivyo na kuanzisha mchakato wa mabadiliko ya sheria ili yawasilishwe katika kikao kijacho cha Bunge.

Alisema ni lazima serikali ifanye uamuzi huo sasa kwa kuwa idadi ya Watanzania imeongezeka hadi milioni 55 na mifugo pia imeongezeka hadi kufikia milioni 35.

Kutokana na ongezeko hilo la watu na mifugo, Rais anasema lipo ongezeko kubwa la mahitaji ya maeneo ya ardhi ikilinganishwa na miaka 50 iliyopita wakati nchi inapata uhuru kwa kuwa wakati huo Watanzania walikuwa milioni tisa na mifugo ilikuwa milioni 10.

**KILIO CHA WANAWAKE**

Ni jambo la kutia huruma unaposikia eti vijiji zaidi ya 300 vitafutwa, hivi wakazi wa maeneo hayo watakwenda wapi? Kina mama na watoto waathirika wakubwa walifikiriwa wangekwenda wapi?

Ina maana wangegeuka kuwa ombaomba barabarani wakiwa na watoto na mafurushi ya nguo na mali zao migongoni? Hivi mabinti zao itakuwaje, hawatasoma tena?

Licha ya kwamba wakiwa vijijini nyumbani kwao hunyanyaswa kijinsia na kupewa mimba za utotoni hivi wakishatimuliwa baada ya kijiji kufutwa ili kuongeza hifadhi wanakimbilia wapi?

Kheee ni kama kuzalisha jeshi la watumishi wa ndani mijini au wauza pombe kwenye baa za pombe za viwandani na mataputapu na vyakula kwa mamalishe? Vipi hatma za kuambukizwa magonjwa yakiwamo ya ngono? Ninyi viongozi mliohusika kubariki kufutwa vijiji na watu kuteseka huwa mnajisikiaje?

Hata hivyo, wanawake wangekuwa na mazingira hatarishi zaidi kwani huenda wangegeuzwa wawindaji wa chakula na chochote kingine kwa njia za aibu au za kuuza miili yao ili wawaponye watoto wao au kujipatia riziki.

Uwezekano wa baadhi ya watoto wa wanavijiji hao kuwa wezi, majambazi , dada poa , hata makontena ya kubeba dawa za kulevya ungekuwa mkubwa . Si hivyo hata uwezekano wa kuwa na idadi kubwa ya wateja na waraibu wa mihadarati ni mkubwa.

Kwa sasa mwelekeo wa serikali na vipaumbele vinajulikana imewekeza kwenye kuwahudumia Watanzania. Habari za mabilioni kuwekezwa kwenye dhifa au ulaji, safari za ng'ambo, mishahara mikubwa, posho na malipo hewa hakuna. La muhimu ni kuwasaidia wananchi maskini hasa hao waliokuwa wahamishwe bila kujua wangeanzia wapi na kumudu vipi maisha yao.

Serikali imefanya maamuzi bora kwa kuwa jumuiya ya waishio kwenye mazingira hatarishi ingeongezeka kwa kufuta vijiji zaidi ya 300, ikumbukwe kuna maelfu ya walemavu, wazee, wagonjwa, wajane na wajawazito ambao wangeumia na kupigika kwa njia mbalimbali.

Ikumbukwe huenda maeneo hayo mwanzoni yalikuwa ya wananchi kabla ya serikali kuyageuza hifadhi, mapori na maeneo tengefu.

# Tanzania inavyopaa Afrika ubora wa vyakula na tiba

Na Mary Geofrey

MAMLAKA ya Chakula na Dawa (TFDA), ni moja ya taasisi za serikali ambazo zinashughulika moja kwa moja na masuala ya uhai wa Watanzania, kwani jicho lake husimamia chakula na tiba ambavyo ni mambo muhimu na mhimili mkuu wa maisha ya wananchi.

TFDA inayosimamiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ndiyo yenye majukumu ya kusimamia viwango vya ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba vyote vinavyotumika nchini.

Majukumu mengine ni pamoja na kudhibiti utengenezaji, uingizaji nchini, usambazaji na utangazaji wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba, kutoa vibali vya kuendesha biashara za bidhaa zinazodhibitiwa na kuzisajili kabla ya kuruhusiwa kuingizwa sokoni.

Katika miaka mitatu ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli, TFDA inaeleza utekelezaji wa majukumu yake na mafanikio yaliyopatikana.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TFDA, Adam Fimbo, katika mahojiano na waandishi wa habari wiki iliyopita anasema, majukumu waliyotekeleza ni udhibiti wa usalama, ubora na usalama wa bidhaa za ndani na nje ya nchi ikiwamo kutambulika kimataifa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya ISO 9001: 2015.

"Hii ni kutokana na mafanikio ya miaka mitatu ya utekelezaji wa kazi chini ya serikali ya awamu ya tano, kwa kufikia na kuvuka malengo tuliyojiwekea katika udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi ili kulinda afya ya jamii nchini," anasema Fimbo.

Mahojiano hayo yalihusisha pia ziara ya maofisa mawasiliano kutoka taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Afya, katika kampeni maalum ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya' inayolenga kueleza mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa awamu ya tano.

"Kutokana na kuwa na mifumo thabiti ya udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa, mnamo Desemba mwaka 2018 TFDA ilitambulika kufikia ngazi ya tatu (Maturity Level 3) ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya ubora wa mfumo wa udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vipodozi, ambapo hatua hii imeifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza barani Afrika kufikia hatua hii," alisema Fimbo.

Anaeleza kuwa, TFDA katika mikakati yake hiyo imeweka mifumo na taratibu za ndani za utoaji huduma na utendaji bora ili kukidhi mahitaji na matarajio ya wateja kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya ISO 9001:2015 kwa huduma za kawaida na ISO 17025:2005 kwa huduma za maabara.

Fimbo anasema huduma za TFDA hutolewa kwa kuzingatia viwango vya Mkataba wa Huduma Wateja kama ulivyorejewa mwaka 2016.

Anasema mfumo huo umeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka



Kaimu Meneja TFDA Kanda ya Kaskazini, Benny John akizungumza na maofisa uhusiano wa Wizara ya Afya na taasisi zake (hawapo pichani) walipotembelea ofisi za mamlaka hiyo, kanda ya kaskazini, jijini Arusha. **PICHA ZOTE: TFDA.**

na idadi ya bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi vilivyosajiliwa imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, katika kipindi cha 2016 hadi 2018.

Anasema bidhaa 14,345 kutoka bidhaa 8,866 zilizokuwa zimesajiliwa mwaka 2015/16 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 62.

"Hii imetokana na kuongezeka kwa uelewa wa matakwa ya sheria miongoni mwa wafanyabiashara na kukua kwa biashara,"anasema Fimbo.

Aidha, TFDA imekuwa ikifanya tathmini na usajili wa bidhaa kwa lengo la kuhakiki endapo bidhaa zinakidhi vigezo vya usalama, ubora na ufanisi kabla ya kuruhusiwa katika soko.

Anasema kuwapo kwa bidhaa nyingi zilizosajiliwa katika soko ni uthibitisho kuwa walaji wanapata bidhaa zilizo salama, zenye ubora na ufanisi.

Fimbo anasema wamesajili maeneo ya biashara za bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi kwa lengo la kutambua maeneo ambayo bidhaa hizo zinazalishwa, kuhifadhiwa, kusambazwa na kuuzwa.

"Mfumo huu husaidia kuhakikisha kuwa maeneo husika yanakidhi vigezo ili kutoathiri usalama, ubora na ufanisi wa bidhaa," anaeleza Fimbo.

Anaeleza zaidi kuwa, TFDA imesajili maeneo 25,630 ya biashara za bidhaa zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na maeneo 9,000 yaliyosajiliwa mwaka 2016/17 na maeneo 5,606 mwaka 2015/16, hii ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 60.5.

"Katika kipindi hiki, TFDA imeendelea kushuhudia kufikiwa kwa dira yake ya kuwa taasisi ya mfano barani Afrika katika udhibiti wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi na hivyo kuvutia nchi mbalimbali kuja kujifunza mifumo iliyopo na kwenda kuitekeleza nchini kwao," anaeleza Fimbo.

Anataja nchi hizo kuwa ni Zimbabwe, Rwanda, Kenya, Uganda, Ethiopia, Sudan Kusini, Botswana, Mauritius, Lesotho na Bangladesh.

Anasema pia katika kipindi cha mwaka 2015/16 hadi 2017/18, mamlaka imefanikiwa kufikia na kuvuka malengo iliyojiwekea katika utekelezaji wa mipango kazi yake.

Mamlaka katika kipindi hicho 18 itaendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji kwa ufanisi wa malengo mahususi nane yaliyomo katika mpango mkakati mpya wa miaka mitano kuanzia 2017/18 hadi 2021/22, ili kulinda afya ya jamii.

Anataja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na kukamilika kwa jengo la maabara na kufungwa kwa vifaa vya kisasa vya uchunguzi jijini Mwanza jambo ambalo limesogeza huduma zaidi kwa jamii.

Anasema pia wameboresha ukaguzi wa shehena za bidhaa zinazoingia na kutoka nchini na kuwezesha kukagua shehena 3,038 ya bidhaa zilizoingia kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2018.

Aidha, shehena 1,494 ya bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vya ndani nchini, zilipitishwa katika mpaka huo kwenda nchi mbalimbali ikiwamo ya Kenya na hivyo kuiwezesha serikali kupata mapato.

**UDHIBITI MIPAKANI**

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa TFDA, Kanda ya Kaskazini, Ben John, akiwa katika mpaka wa Namanga mkoani Arusha katika ziara ya Maofisa Mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, anasema wamefanikiwa kudhibiti bidhaa zinazoingia nchini kiholela kupitia mpakani.

Anasema imeboresha ukaguzi wa shehena za bidhaa zinazoingia na kutoka nchini na kuwezesha kukagua sheheha 3,038 ya bidhaa zilizoingia kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2018 katika mpaka huo.

"Udhibiti wa bidhaa zinazoingia nchini umeongezeka kwa kuwabana wafanyabishara waliokuwa wanakwepa kulipa kodi na tozo za serikali na hivyo kuongeza pato la taifa. Mfano bidhaa zilizoingia nchini mwaka 2016 ni shehena 754, mwaka 2017 shehena 1,061 na mwaka 2018 shehena 1,223," anasema John.

Anasema pia bidhaa zilizodhibitiwa na TFDA na zilizosindikwa kwenye viwanda vya ndani kwa muda wa miaka mitatu zinaongezeka na kwamba mwaka 2016 zilikuwa shehena 429, mwaka 2017 shehena 425 na mwaka 2018 shehena 640.

Aidha, TFDA imepunguza upotevu wa fedha za kigeni zinazotokana na uingizaji holela wa bidhaa zisizofaa au zile za magendo kwa kudhibiti mianya ya wafanyabiashara wasiyo waaminifu katika kanda hiyo ya Kaskazini.

"Thamani ya bidhaa zilizokamatwa zikiingizwa nchini pasipo kufuata taratibu imepungua kutoka Sh. milioni 630.3 mwaka 2016 hadi Sh. milioni 24.7 mwaka 2018," anasema John.

Anasema hayo yote yamewezekana kutokana kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji kazi katika mpaka huo, katika kudhibiti ubora wa bidhaa na usalama wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.

Kwa upande wake, Mkaguzi Mfawidhi wa TFDA katika mpaka huo, Elia Nyeura, anasema kutokana uboreshaji wa utendaji kazi umewezesha udhibiti wa bidhaa zilizokuwa zinapitishwa kwenye njia za panya.

Anasema pia wameongeza idadi ya watumishi wanaotenda kazi kwa ufanisi na kwa muda mfupi katika kuhakikisha wanalinda afya za walaji na watumiaji wa dawa nchini. Nyeura anasema katika utekelezaji wa majukumu yao wanashirikiana na maofisa wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali(GCLA), Shirika la Viwango nchini (TBS) na Jeshi la Polisi.



Ofisa Ukaguzi wa TFDA Titus Malulu, akionyesha maabara inayohamishika wanavyoitumia kukagua dawa,vifaa tiba pamoja vitendanishi katika kituo cha ukaguzi kilichopo kati ya mpaka wa Kenya na Tanzania cha Namanga.

HABARI KIMATAIFA

# AU yataka Congo isitoe matokeo ya uchaguzi

**ADDIS ABABA, Ethiopia**



UMOJA wa Afrika (AU) umetoa wito kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kuahirisha utoaji wa matokeo rasmi ya uchaguzi wa rais ambayo bado yanazozaniwa, kutokana na kuwepo na wasiwasi juu ya matokeo ya awali.

Umoja huo uliokutana Alhamisi wiki hii Addis Ababa, Ethiopia, ulihitimisha kwamba kulikuwa na "wasiwasi mkubwa katika ulinganifu wa matokeo ya awali, kama yalivyotolewa na tume huru ya uchaguzi CENI.

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Dk. Moussa Faki Mahamat, (pichani), alisema "hata hivyo, ingawa hali nchini humo imebaki kuwa tulivu hadi sasa, lakini inatia shaka. Ili kuliweka wazi, kuna wasiwasi mkubwa juu ya ulinganifu wa matokeo yaliyotangazwa, yanayoendelea kugonga vichwa vya wacongomani na ndugu zao wote kote duniani," alisema Mahamat.

Hoja hiyo ya nadra kutoka Umoja wa Afrika inaibua wasiwasi mpya katika mchakato wa baada ya uchaguzi, ambao ulikuwa na maana ya kulivusha taifa hilo kwa mara ya kwanza katika kukabidhiana madaraka kidemokrasia ndani ya miaka 59 ya uhuru, lakini limejikuta katika mkwamo tangu kura ya Desemba 30.

Matokeo rasmi yanatarajiwa kutolewa na tume ya uchaguzi siku ya Ijumaa mara baada ya mahakama ya katiba kutolea uamuzi changamoto zilizowasilishwa baada ya matokeo ya awali kutangazwa. Lakini Umoja wa Afrika unataka matokeo rasmi yasitangazwe kufuatia wasiwasi uliopo.

Msemaji wa serikali ya Congo Lambert Mende, amelaani kauli hiyo ya Umoja wa Afrika, akisema mahakama inayochunguza uhalali wa kura ilikuwa "huru". "Sidhani ni wajibu wa serikali au Umoja wa Afrika kuieleza mahakama ya katiba nini cha kufanya".

Vyombo vya habari kadhaa vya kimataifa siku ya Jumanne wiki hii viliripoti kwamba taarifa za kura zilizovuja zilionyesha mgombea wa upinzani Martin Fayulu, ndiye aliyeshinda katika uchaguzi uliofanyika Desemba 30.

Kituo cha Utangazaji cha Ufaransa RFI, gazeti la Uingereza la Financial Times, na televisheni ya TV5 Monte, ziliripoti kwamba taarifa za kura zilizovuja, ambazo hazichapishwa zinaonyesha mgombea aliyetangazwa na tume ya uchaguzi Felix Tshisekedi hakushinda.

Fayulu alidai kulikuwa na udanganyifu na tayari amepeleka shauri kwenye mahakama ya juu akitaka kura zihesabiwe upya.

Anapendekeza kwamba Tshisekedi na Rais Joseph Kabila walifikia makubaliano baada ya matokeo ya awali kuonyesha mgombea kutoka chama tawala Emmanuel Ramazani Shadary aliibuka nafasi ya tatu.

Mapema wiki hii Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika SADC, iliondoa shinikizo lake dhidi ya mamlaka ya Congo ambapo awali iliunga mkono wito wa kura kuhesabiwa tena.

*DW*

# Trump, Spika wanazidi kuzozana

**WASHINGTON, Marekani**

UHASAMA kati ya Rais Donald Trump na Spika wa Baraza la Wawakilishi Marekani, Nancy Pelosi umezidi kupamba moto baada ya Trump kumzuia Pelosi kutumia ndege ya kijeshi kwa safari yake ya kikazi ya kwenda Afghanistan.

Mzozo baina ya viongozi hao wa Marekani umezidi makali baada ya Nancy Pelosi, ambaye ni spika wa Baraza la Wawakilishi, kupendekeza kwamba Rais Donald Trump aahirishe hotuba yake ya hali ya taifa, ambayo ilikuwa itolewe January 29, kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha za maandalizi.

Trump alimjibu Pelosi kwa barua, na kumwambia kuwa naye hana ruhusa ya kutumia ndege ya serikali kwa safari yake ya kwenda Afghanistan.

Trump alisema safari hiyo ni shughuli inayohusu mahusiano ya umma licha ya kwamba hata yeye binafsi alifanya ziara ya aina hiyo katika eneo lenye vita. Trump alisema itakuwa vyema kwa Pelosi kubaki Marekani na kujadili suala la kufungua tena shughuli za serikali.

Kumnyima mbunge wa ngazi ya juu ndege ya kijeshi, achilia mbali Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye ni wa pili kwa cheo katika Serikali ya Marekani, ambaye anataka kutembelea eneo la vita ni kitu cha nadra sana kutokea. Wabunge walishangazwa na uamuzi huo. Msemaji wa Pelosi Drew Hammill, alisema spika huyo alipanga kwenda Afghanistan na Brussels, kuwashukuru wanajeshi kwa huduma yao, na kupokea taarifa kutoka kwa wanajeshi walio huko juu ya usalama wa taifa na taarifa nyingine za upelelezi.

Hammill alimkumbusha kwamba Trump alisafiri kwenda Iraq wakati tayari shughuli za serikali zikiwa zimeshafungwa.

Aidha, Rais Trump alisema, shughuli za serikali zitaendelea kufungwa hadi Baraza la Congress limpatie dola bilioni tano ili ajenge ukuta katika mpaka wa Mexico na Marekani. Nancy Pelosi alisema yuko tayari kujadili suala la fedha za kuimarisha usalama katika mpaka wa Marekani na Mexico mara baada ya shughuli za serikali kufunguliwa tena, lakini aliongeza kuwa wabunge wa chama Democratic wamesema bado wanapinga mpango wa Trump wa kujenga ukuta.

*DW*

## Wanaanga China Wafanikiwa kuotesha mmea mwezini

**BEIJING, China**

MMEA uliopandwa na wanaanga wa China mwezini umechukua takriban siku nane kuota. Chombo cha angani cha China kwa jina la Change4 kiliacha kunyunyuzia maji mbegu hiyo ya pamba kama ilivyopangwa na Chuo Kikuu cha Chongqing ambacho kiliandaa jaribio hilo.

China ilipanda mmea wa kwanza mwezini na kueleza kwa nini ni muhimu kuendelea na uchunguzi angani, kuotesha mimea huo unalenga kuwapunguzia wataalamu safari zakurudi duniani kutafuta vyakula.

Mmea huo uliota katika chombo ndani ya Change4 ambacho kilitua katika eneo la mbali na mwezini mnamo Januari 3, mwaka huu.Eneo ambalo mmea huo ulikulia usingeweza kuishi katika usiku wa mchana wakati wa kupatwa kwa mwezi.

Wakati huo wote wataalamu wa China watalazimika kulala na mifumo yao yote italala ili kuhifadhi nishati. Ilielezwa kuwa hivyo basi mmea huo haukunyunyuziwa maji na ulikufa , kama ilivyokuwa imepangwa.

Majaribio mengine

Chombo hicho cha China pia kilibeba mbegu za viazi na 'arabidopsis' mmea kutoka jamii ya haradali pamoja na matunda na mayai ya chuchu.

Ilitarajiwa kuwa nyuzi joto duniani zitashuka hadi kipimo cha nyuzi 52 ili viumbe hao wagande, chuo hicho kilisema katika taarifa iliyotolewa Jumanne kwamba wakati nyuzi joto zinapoanza kupanda mwezi ujao, viumbe vitaruhusiwa kuoza katika chombo kilichofunikwa kikamilifu.

Baadhi ya matokeo yalishangaza matarajio yalielezea mtaalamu na mwanzilishi wa jaribio hilo , Xie Gengxin, katika runinga ya China.

Alisema uwezo wa kupanda mimea mwezini ni muhimu katika uchunguzi wa siku zijazo angani na kwamba ziara kama vile za sayari ya Mars ambayo itachukua takribani miaka miwili na nusu kuwasili inakokwenda.

Hiyo itamaanisha kwamba wanaanga wataweza kupanda vyakula vyao angani , wakipunguza haja ya kurudi duniani ili kubeba chakula zaidi.

Katika jaribio hilo imebainika kuwa kuna jitihada za kuutumia mwezi kama kituo husuan kwa safari za kuelekea sayari ya Mars kwa kuwa ni karibu na duniani.

**BBC**

# HADITHI

AJALI kubwa iliyotikisa nchi inatokea eneo la Mikese mkoani Morogoro baada ya basi la abiria kuungua moto, kuua na watu wengine kujeruhiwa.
Awali inachukuliwa poa kama ajali za kawaida. Lakini nyuma ya pazia, ni ajali iliyopangwa na muuaji , mwenye akili za kiwendawazimu, akibebwa na hisia za chuki, wivu na kisasi bila kujali madhara kwa watu wengine wasiohusika. Eddy Kamal, mpelelezi makini, anategua kitendawili hiki. Fuatilia kisa hiki....

# Kisanduku Cheusi-31

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**



MLINZI yule aliona kama kuna kitu kimerukia ndani. Akili yake iliona kabisa kuwa haikumdanganya. Alichokiona ni kitu halisi. Ingawa hakujua kama ni binadamu, mnyama au mzigo.

Taratibu alianza kunyata kuelekea pale alipoona kuwa kile kitu kimengu-ka. Sehemu yenyewe ilikuwa na nyasi nyingi. Eddy naye aligundua kuwa kuna mtu ananyemelea eneo ambalo ameangukia.

Kwa bahati nzuri halikuwa likipigwa na mwanga wa taa, hivyo kulikuwa na giza kidogo. Alikuwa amelala na kunyooka bila kutikisika mithili ya mti.

Kwa tahadhari ya hali ya juu, mlinzi aliinua bunduki yake na kuikoki, akitanguliza mbele, vidole vyake vikiwa tayari kufatua iwapo atagundua kuna chochote kile ambacho hakikutakiwa kuwepo pale.

Eddy alikuwa ametulia tuli akisaidiwa na giza. Nguo alizovaa zilimpa tabu mlinzi kumuona. Ghafla kama chui, aliruka na kumkamata mlinzi kwa nyuma, akambana ili asigeuke.

Kwa haraka ile ile alipiga teke vidole vya mlinzi na kumfanya ahisi maumivu makali yaliyofanya kuichia bunduki.

Alimkaba kabari ambayo ilimmaliza nguvu na kumfanya asalimu amri kuelekea kwenye ardhi.

Eddy hakutaka kumuua, bali kumfanya azirai kwa muda.

Alichofanya kilifanikiwa kwa asilimia nyingi tu, bila mtu yoyote yule kwenye jengo lile kugundua.

Alipohakikisha kuwa amefanikiwa kufanya alichotaka kukifanya, alielekea alikotaka kwenda.

Alipita mle mle ambako alipitia mwanzo wakati anatoka. Mwishoni aliteremka kwenye chumba chake alichowekwa kama mahabusu.

Alipohakikisha ameweka 'ceiling board' vizuri kana kwamba hakukuwa na kitu chochote kibaya, alianza kukagua kuona kama huenda kulikuwa na mtu alikuwa ameingia mle ndani na kumkosa.

Kila kitu kilienda sawa. Hakukuwa na dalili ya kiumbe chochote kuingia chumbani mle wakati yeye alipofanya ziara nje.

Alichofanya sasa ni kuanza kazi. Alikusanya vitu vyote alivyoingia navyo mle ndani ambavyo aliona kuwa vitamsaidia, zikiwemo silaha ndogo zenye uwezo wa kufichwa bila kuonekana, rediokoli ndogo, pamoja, kamera, kinasa sauti na vitu vingine ambavyo aliona vitamfaa.

Alivificha sehemu ambayo ni mtalaam pekee ndiye anaweza kuvumbua.

Saa yake iliyomuonyesha kuwa sasa ni saa 9:30 usiku. Kulishaanza kucha.

Ni masaa machache tu kuingia siku mpya. Siku ambayo yeye amepangiwa kuuawa ndani ya jengo hilo na maiti yake kuzikwa humo humo na kutoonekana milele.

Kutokana na safari ya usiku aliyoifanya, alishikwa na uchovu akapata usingizi.

Aliamshwa na kufunguliwa kwa mlango. Kama kawaida aliyeingia alikuwa ni kijana wa siku zote ambaye alikuwa anamletea chai.

Tayari walikuwa wamezoeana na kijana huyo, kiasi cha siku hiyo kumpa gazeti asome.

Alipitia kurasa mbili tatu za gazeti la Nipashe, akamrudishia na kuanza kunywa chai na vipande vinne vya mkate mkavu.

Ilipotimu saa 8:00 mchana, mlango ulifunguliwa. Aliyeingia alikuwa ni baunsa akiwa na mtu mmoja ambaye Eddy hakupata kumuona.

"Wewe si unajifanya mjanja, leo nitamwambia bosi atuachie ukumbi tupigane nione, maana unajifanya unaziweza." Baunsa alipigwa mkwara.

Eddy hakujibu chochote na hakuwa na haja ya kujibu. Akili yake ilikuwa ikijiuliza ni wapi anapelekwa.

Lakini alijua popote pale anapolekewa wakati huo, si kwenda kuuawa kwa sababu aliambiwa kuwa atauawa usiku.

Pia uzoefu wake wa kazi huo, hajawahi kuona mtu yoyote anayeuawa kwa kupangwa akiuawa mchana.

Ziara hiyo iliishia kwenye chumba kimoja ambacho hajawahi kukiona wala kupelekwa tangu awe mle ndani kwa siku nne sasa.

Kilikuwa chumba chenye hadhi ya kuitwa chumba. Kilikuwa na kila kitu kana kwamba ni nyumbani kwa mtu.

Alionyeshwa kwa kukaa. Waliomleta walikaa pembeni yake. Dakika tano baadaye aliingia mtu ambaye hakuwa mgeni kwenye macho ya Eddy.

Ni kijana mrefu wa wastani mkakamavu, asiyezidi umri wa miaka 35 hivi.

Sura, mavazi na muonekano wake ulionyesha kuwa mtu mwenye neema.

Yaani alikuwa na uwezo wa kifedha au hali nzuri kimaisha.

Hakuwa mwingine bali ni Benson Mapunda. Aliingia akiwa kama ameingia ofisini. Alikuwa ameshika karatasi kadhaa na makabrasha.

Alikaa kwenye kiti kilicho tofauti na vile vilivyomo kwenye chumba hicho kilichokuwa na kiyoyozi. Kiti hicho kilikuwa na thamani zaidi.

> **"Mimi ndiye mmiliki wa Paradise Hoteli. Miaka kadhaa nyuma nilimpokea mrembo mmoja anaitwa Careen. Alikuja kuomba kazi baada ya kumaliza kozi ya uhotelia. Kwa jinsi alivyo mrembo nilimpa kazi haraka sana. Lakini pia nilimpenda na akawa mpenzi wangu.**

Alianza kukagua karatasi kadhaa kana kwamba alikuwa naziaona kwa mara ya kwanza.

"Leo ndiyo siku ile ambayo tumeipanga na wenzangu." Benson alianza.

"Ni siku ambayo kwangu mimi itakuwa na maana sana, maana nitamaliza mzizi wote wa fitina ambao kwa zaidi ya mwaka ulikuwa unanitesa sana." Benson alikuwa akiwaambia kiasi cha watu wanane waliokuwa ndani mle akiwemo Eddy.

"Nitammaliza, au nitamuua mtu ambaye amesababisha matatizo yote haya yaliyonipata hadi nimefanya mambo mengi na kutumia gharama nyingi. Nimeua watu wengi ambao wengine walistahili na wengine hawakustahili kwa sababu ya mwanamke mmoja tu aitwaye Careen." Alinyamaza na kunong'oneza mmoja wa wasaidizi wake ambaye alitoka kidogo na ndani ya dakika moja alirejea na chupa ya maji.

Alifungua na kummiminia bosi wake kwenye glasi. Banson alinyanyua na kunywa mafunda kadhaa akaweka glasi kwenye meza.

"Siri hii nimeificha kwa muda mrefu na wasaidizi wangu wengi walichokuwa wakikifahamu ni kupokea maagizo tu ya kufanya, kamate fulani, hakikisha fulani anafuatiliwa, hakikisha kesho anakufa, lakini hakuna aliyekuwa akifahamu kisa. Leo aliyesababisha yote haya yupo hapa na leo hii atakufa mbele yenu na kuzikwa humu humu ndani, hivyo hadithi, tamthilia au filamu yangu mimi na Careen itakuwa imeishia hapa, nitaanza maisha mengine mapya, kwani tayari nimeshampata mpenzi mwingine anaitwa Lisa.

Wapendwa wafanyakazi wangu, huku aliyekuwa mbele yenu anaitwa Peter Mayambua. Ndiye aliyekuwa anataka kumuoa Careen. Ndiye aliyemrubuni mpenzi wangu akanikataa na kutaka kuolewa na huyu paka." Alisema na kusababisha wenzake wacheke.

Pamoja na Benson kuonyesha hasira, kitu kimoja ambacho Eddy alikuwa akimsifu kimoyomoyo ni kutomtesa, kwani siku zote hizi hakupata kuteswa au kipigwa, ingawa jamaa huyo alikuwa akionyesha wivu wa wazi wazi tangu alipogundua kuwa yule aliyefika kwenye ofisi yake siku ile ni Mayambua na ndicho kilichosababisha atekwe.

"Samahani bwana Mapunda katika hili mimi naweza kuuliza maswali?"

"Nilisema kuwa kabla sijakuua nitaeleza kila kitu kwako na hata wafanyakazi wangu kila kitu kilichofanywa kuanzia Careen kuuawa hadi kukamatwa kwa wewe mchumba wake. Furaha yangu leo ni kuona wewe unauawa mbele yangu na Careen ameuawa na mimi baada ya wiki moja namvisha pete mchumba wangu Lisa."

"Mimi ndiye mmiliki wa Paradise Hoteli. Miaka kadhaa nyuma nilimpokea mrembo mmoja anaitwa Careen. Alikuja kuomba kazi baada ya kumaliza kozi ya uhotelia. Kwa jinsi alivyo mrembo nilimpa kazi haraka sana. Lakini pia nilimpenda na akawa mpenzi wangu.

Baada ya mwaka mmoja tu akaniambia kuwa ana ndugu yake, pacha mwenzake walikuwa naye kozi moja naye anataka amlete hapo. Hakukuwa na pingamizi, akaletwa Hellen."

Jina la Hellen lilisababisha Eddy kupatwa hasira, lakini iliyoishia tumboni, kwani alijua kabisa kuwa kifo cha mpenzi wake kilitokana pia na hila za Benson. Alijipanga pia kumuuliza juu ya kifo cha Hellen jinsi kilivyokuwa.

*Itaendelea Jumamosi.*

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KADI YA GARI IMEPOTEA

**MAJUTO JAPHARY BASHIR,** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Yenye namba za usajili **T 531 CJR,** aina ya **TOYOTA IST** Chassis namba: **NCP600151270,** Engine namba. 2NZ741,

Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa Polisi:
**URP/RB/324/2019**

115015102

### VYETI VIMEPOTEA



**EDWARD CHIAGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0564.0152** kilichotolewa na BUSWELU SEKONDARI mwaka 2012. Cheti cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) RWAMKOMA (822 KJ) mwaka 2015. Cheti cha Darasa la Saba Shule ya Msingi JITIHADA mwaka 2008. Cheti cha kuzaliwa.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa ya polisi: MW/RB/6841/2018.**

115013602

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**PETER ANDREW HELLAR,** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Yenye namba za usajili **T198 DKM** aina ya **TOYOTA CROWN** Chassis namba: **GRS200010882**, Engine namba.2480,

Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

**Taarifa Polisi: RB/95386/18**

215015002

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya mwanzo
Hai KATI
Usimamizi wa mirathi namba .....2...mwaka .......2019.....................
Ombi la FATUMA HAMISI SIDI kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAMISI ALLY SIDI

Watu wote mnaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka,mnamo tarehe 24-01-2019 Kabla ya huyu mwommbaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyu upo mahakamani waweza kukaguliwa.
Imetolewa leo 17-01- mwaka 2019

SAHIHI YA HAKIMU

115014302

### KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MARTIN MBONEA MZIRAY.** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya STAR Yenye namba za usajili **MC 320 BAF** Chassis namba **LTZHCM-LA4BF1000018.** Engine namba **163FMLB0002018.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/72/2019.**

115014402

### KUPOTEA KWA KADI YA TRAILER

**ZASH COMMERCIAL SERVICES AFRICA LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya Trailer yenye namba za usajili **T 375 CAA. CHASSIS NO; A068296.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**CD/TR/RB/4040/2018.**

115014802

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GABRIEL BENARD** SHAMBA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 936 DGB TOYOTA HIACE.** CHASSIS NO; **RZH1830001251.** ENGINE NO; **3L9153215.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KJN/RB/910/2019.**

215013402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo: SANYA JUU (W) SIHA Usimamizi wa Mirathi No. 2/2019 Ombi la ANTHONY GOODLUCK SHUMA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu FEDILIA TIMONTHY SHUMA KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 8/2/2019.

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 8/1/2019

Sahihi ya Hakimu.
HAKIMU MKAZI.
MAHAKAMA YA MWANZO
SANYA JUU

215014102

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SPANISH TILES AND SANITARY WARES LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T 838 ARM.** Chassis namba **LH1190083576.** Engine namba **3L4183808.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**
**OB/RB/583/2019.**

115011702


*Uza, Chenye Thamani Kubwa*


## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

## Nipashe

NI JIBU LAKO, NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# UNAI:

## Ozil anaweza kuivaa Chelsea

**LONDON, England**

UNAI Emery amedai kwamba hafikirii uwezekano wa kuondoka kwa Mesut Ozil na amedokeza kwamba Mjerumani huyo anaweza kurudi kwenye kikosi kwa mara ya kwanza leo Jumamosi, wakati washikabunduki hao wanapocheza na Chelsea.

Majaliwa ya Ozil yamekuwa gumzo katika wiki za hivi karibuni huku ripoti zikidai kuwa mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid anaweza kuondoka hapo kwenye Uwanja wa Emirates, huku Inter ikitajwa kumwania.

Imeripotiwa kwamba Ozil haonekani kama mchezaji muhimu wa Arsenal kwa zama hizi za Emery na bosi huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain anaweza kufikiri kumuuza ili kupata fedha za kununulia wachezaji wengine.

Ozil alikosa mchezo wa Arsenal ikifungwa 1-0 na West Ham wikendi iliyopita, akitajwa kuwa ni majeruhi, lakini Emery amethibitisha kwamba kiungo huyo amefanya mazoezi na kikosi hicho na anaweza kuwepo kwenye mchezo wa wikendi hii.

Akizungumza kabla ya mchezo huo, Emery alisema: "Alikuwa na majeruhi, na kuna kitu kipo sawa na anaweza kucheza.

"Nataka kila mchezaji kuwa sawa kwa ajili ya kila mchezo na yeye yupo hivyo. Hakucheza mchezo uliopita, lakini Jumamosi hii anaweza kuwa na sisi."

Emery pia alikanusha taarifa kwamba amezungumzia kuondoka kwa Ozil, akiongeza: "Sifikirii kuhusu hilo. Nafikiri kwa namna gani anaweza kutusaidia.

"Kuna wakati alitusaidia kwa kiwango chake kizuri dimbani na wengine kutofanya vizuri. Baada ya wiki hizi mbili, pengine anaweza kuwa sawa na sisi."

Wakati uvumi ukienea kwamba Ozil anaweza kuondoka mwezi huu au kipindi kijacho cha majira ya joto, lakini wakala wake amedai kwamba mteja wake anataka kubakia hapo kwa washikabunduki hadi mwisho wa mkataba wake mwaka 2021.

# DZEKO

## KUTUA WEST HAM

**LONDON, England**



KLABU ya West Ham United imehusishwa na uwezekeno wa kumsajili mshambuliaji wa AS Roma, Edin Dzeko, wakati wakitafuta mrithi wa nyota wao anayetaka kuondoka wakati huu wa Januari, Marko Arnautovic.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Bosnia amefunga mabao saba katika michuano yote kwa Giallorossi hao msimu huu, bado amekuwa katika wakati mgumu kupata namba ya kudumu kwa kikosi cha kocha, Eusebio Di Francesco.

Mfungaji bora wa Wagonga nyundo hao wa London, Arnautovic anaonekana anaweza kuondoka kwenye klabu hiyo wiki mbili zijazo, baada ya wakala wake kuishutumu klabu hiyo kwa kukataa ofa ya paundi milioni 35 kutoka kwa klabu ya nchini China ya Shanghai SIPG, akibainisha kwamba mchezaji huyo raia wa Austria anataka kuondoka hapo kwenye dimba la London.

Kwa mujibu wa ripoti ya gazeti la Daily Star, Roma wapo tayari kumruhusu Dzeko kuondoka wakati wa dirisha la Januari wakati wakiangalia namna ya kukiboresha kikosi chao.

Kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 atajiunga na West Ham atajiunga na kocha wake wa zamani, Manuel Pellegrini.

Dzeko alicheza mara kwa mara wakati kocha huyo raia wa Chile alipokuwa akiionoa Manchester City na alifunga mabao 16 kwenye Ligi Kuu msimu wa 2013/14, akiisaidia timu hiyo kuifunga Liverpool na kutwaa ubingwa.

# MOURINHO: NILIMPENDA MO SALAH

**LONDON, England**



JOSE Mourinho amezungumzia uhusuano wake na Mohamed Salah aliyekaa kwa muda mfupi Chelsea, huku akisisitiza kwamba yeye hakuhusika kwa namna yoyote ile kumfanya nyota huyo wa sasa wa Liverpool aondoke Stamford Bridge.

Salah alijiunga na Mourinho pale Chelsea Januari mwaka 2014 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 11, lakini alishindwa kupenya katika kikosi cha kwanza na akapelekwa kwa mkopo Fiorentina wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Mchezaji huyo wa Misri aliweza kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu Italia maarufu Serie A, na akarudi England msimu wa 2017/18, akifunga mabao 32 katika mechi 38 za Ligi Kuu akiwa na Liverpool.

Mara kwa mara Mourinho amekuwa akilaumiwa kwa kumbeza Salah, huku wangine wakidai kwamba Mreno huyo hakumpa nafasi Salah na hivyo kulazimika kuondoka hapo Chelsea.

Hata hivyo, akizungumza kwa mara ya kwanza na beIN Sports tangu alipofukuzwa kama kocha pale Manchester United, Mourinho alikataa madai hayo, akidai kwamba alikuwa na 'mapenzi' mema na Salah.


Mourinho alisema: "Nilicheza dhidi ya Basel kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Salah alikuwa mtoto pale Basel. Na nilimpenda. nikamnunua.

"Niliomba klabu imnunue yeye na tayari wakati huo tulikuwa na safu imara ya washambuliaji, Hazard na Willian, na tulikuwa na vipaji vikubwa pale.

"Lakini niliwambia wamnunue mtoto yule. Alikuwa akicheza zaidi kama winga kuliko mshambuliaji."

Mwaka 2013, wakati akiwa na Basel, Salah alifunga mabao matatu katika mechi nne alizocheza dhidi ya Chelsea.

# TOTTENHAM
## YAJITOSA KUMSAJILI MALCOM



**LONDON, England**

KLABU ya Tottenham imeripotiwa inafanya makubaliano na Barcelona juu ya winga wa Brazil, Malcom, wakati wakiangalia uwezekano wa kumsajili kwa mkopo kabla ya kufungwa kwa dirisha hilo dogo la usajili.

Spurs imekuwa ikihusishwa na washambuliaji kadhaa kwenye siku za hivi karibini, na sasa uvumi umeenea zaidi baada ya kuumia kwa mshambuliaji wake, Harry Kane.

Kwa mujibu wa magazeti ya nchini Hispania, Spurs inataka kumsajili Malcom, ambaye alisajiliwa hapo Barcelona kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Ripoti zinadai kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alijiunga na Barcelona akitokea Bordeaux kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 41.

Hata hivyo, nyota huyo amekuwa kwenye wakati mgumu wa kupata namba katika kikosi cha kwanza hapo Camp Nou, akicheza mechi kumi tu kwenye mashindano yote.

Tottenham sasa inafikiri kumsajili mchezaji huyo hapo London Kaskazini baada ya Kane kukumbwa na majeruhi wakati wakifungwa 1-0 na Manchester United Jumapili iliyopita.

Hata hivyo, Spurs inakabiliwa na upinzani kutoka kwa klabu nyingine ambazo nazo zinamwania mchezaji huyo.

Baadhi ya klabu hizo ni pamoja na ile ya Ligi Kuu ya China, Guangzhou Evergrande, ambayo ilitoa ofa kubwa kwa Malcom mwezi uliopita.

Wakati Barca ikiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, Malcom ameshindwa kuwa na manufaa yoyote kwa klabu hiyo msimu huu kwa Blaugrana hao.

Alifunga mabao mawili, amecheza kwa dakika zote 90 mara moja tu kwenye Kombe la Copa del Rey raundi ya 32 katika mchezo wa pili.

Malcom alitua barani Ulaya akitokea Brazil mwaka 2016, baada ya kucheza kwa misimu minne na Corinthians.

Alijiunga na miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Bordeaux, ambapo aliwasaidia kumaliza katika nafasi ya sita mara mbili mfululizo.

Hata hivyo, tangu kipindi cha majira ya joto alikwenda Hispania kwa ajili ya kutafuta nafasi zaidi, na alicheza kwenye kikosi cha Barca kilichocheza juzi Alhamisi dhidi ya Levante.

## ROBERTSON AJIFUNGA LIVERPOOL HADI 2024

**LIVERPOOL, England**

BEKI wa pembeni wa Liverpool, Andy Robertson ameongezewa mkataba mpya baada ya kuonyesha kiwango kizuri, ambao utamfanya akae hapo Anfield hadi mwaka 2024.

Robertson amekuwa na kiwango kizuri hapo tangu alipojiunga akitokea Hull City wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2017.

"Haraka klabu iliponifuata, sikuikatalia, nataka kukaa hapa, na waliponipa ofa niliisaini haraka," alisema Robertson akiiambia tovuti ya Liverpool.

"Ulikuwa mkataba mzuri na rahisi kwa upande wangu na nina uhakika kwa klabu pia. Wote tulikubaliana haraka, ndio maana imefanyika haraka."

Robertson amekuwa mchezaji wa kwanza hivi karibuni wa Liverpool kukubali kusaini mkataba mpya, baada ya Roberto Firmino, Sadio Mane, Mohamed Salah na Joe Gomez kufanya hivyo mwaka jana.

Beki mwingine wa pembeni wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold, anatarajia kufuata nyayo hizo kwa kusaini mkataba wa kuendelea kufanya abakie hapo.






## VALENCIA ANATAKA KUMALIZIA SOKA UNITED

**MANCHESTER, England**

NAHODHA wa Manchester United, Antonio Valencia ameripotiwa kwamba anafikiri kumaliza muda uliobaki kwenye mkataba wake na klabu hiyo, licha ya kutokuwa katika kikosi cha kwanza chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Valencia amejikuta mwenyewe akiwa chaguo la tatu kama beki wa kulia dhidi ya Ashley Young na Diogo Dalot, na ameanza katika mechi moja tu kati ya sita tangu kutua kwa Solskjaer.

Huku mkataba wake ukiwa unamalizika wakati wa kipindi kijacho cha majira ya joto na kulikuwa na uvumi kwamba anaweza kuondoka wakati huu wa dirisha dogo la usajili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 ameithibitishia klabu hiyo kupitia wawakilishi wake kwamba hana mpango wa kuondoka, na angependa kupata mkataba mpya ili amalize kipindi chake cha uchezaji akiwa na klabu hiyo.

Kama United wanaweza kulikubalia ombi lake au kulikataa hilo ni suala la kusubiria, huku klabu kadhaa barani Ulaya zikitajwa kuwania nafasi yake.

Inter ni moja ya klabu ambazo zinazomwania beki huyo wa kulia ambaye amaichezea klabu hiyo jumla ya mechi 300 United tangu alipojiunga nayo akitokea Wigan mwaka 2009.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RASHFORD KULIPWA MSHAHARA MNONO

●●●Lengo ni kuinyima nafasi Madrid na klabu nyingine zinazotaka kuwania saini...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inapanga kumwongezea mara mbili zaidi mshahara wake, Marcus Rashford na kuwa pauni 150,000 kwa wiki, ikiwa ni ofa waliyoitoa kwa ajili ya kumpa mkataba mpya wa kuendelea kubakia hapo Old Trafford.

United imetoa ofa hiyo kwa Rashford baada ya mchezaji huyo kuonyesha kiuwango kikubwa cha juu kwenye kikosi hicho tangu kuwasili kwa kocha wa muda, Ole Gunnar Solskjaer.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England amefunga mabao sita na kutoa 'asisti' tatu katika mechi zake tisa zilizopita za United na sasa wanataka kumzawadia mkataba mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 awali alikuwa akilipwa mshahara wa pauni 75,000 kwa wiki, huku kukiwa kumebakiwa na miezi 18 katika mkataba wake na sasa atalipwa kiasi hicho cha pauni 150,000, kwa mujibu wa gazeti la The Mirror.

Ingawa klabu hiyo ilikuwa na kipengele cha mkataba wake na mchezaji huyo wa kuongeza mwaka mmoja, lakini sasa wanataka kumpa mkataba wa muda mrefu.

Kupewa mkataba huo mpya ni sehemu pia ya kumfunga kutokana na ofa kutoka Real Madrid ambaye imekuwa ikimuwania.

Rashford atafikisha mechi 150 kuichezea United wakati watakapoivaa Brighton leo kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Mchezo huo utakuwa ni wa saba kwa Solskjaer ambaye ameshinda mechi zake zote sita, huku Rashford amekuwa mchezaji muhimu katika safu ya ufungaji wa mabao ambaye alisajiliwa na Louis van Gaal mwaka 2016. Rashford alifunga bao la ushindi na pekee kwenye mchezo dhidi ya Tottenham kwenye Uwanja wa Wembley Jumapili iliyopita na pia alifunga bao la ushindi dhidi ya Newcastle mapema mwezi huu.

Ukiacha Madrid klabu ya Juventus pia imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili Rashford, hivyo kupewa mkataba huo mpya kutazima ofa kutoka kwa klabu hizo.

Nyota huyo ni zao la akademi ya United, alionekana kuwa na wakati mgumu chini ya kocha wa zamani, Jose Mourinho.

Lakini sasa mambo yanaonekana kumnyokea akiwa ndiye chaguo la kwanza chini ya kocha, Solskjaer.

Baada ya kufunga mabao manne tu katika mechi 20 kwenye msimu wake wa kwanza chini ya Mourinho, Rashford amefunga mara nne katika mechi sita chini ya Solskjaer.

Mchezaji huyo wa England amekuwa akiongoza kwenye safu ya ufungaji mbele ya Romelu Lukaku.

## KWA UFUPI

**RAMSEY, JUVE KIMEELEWEKA**
AARON Ramsey amesaini mkataba wa awali wa makubaliano ya kujiunga na Juventus akitokea Arsenal katika kipindi cha majira ya joto. Kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Wales mwenye umri wa miaka 28 amefuzu vipimo vya afya kwa ajili ya kuanza kuwachezea mabingwa hao wa Serie A vilivyofanyika mwishoni mwa wiki. ***(Sky Sports)***

**HUDSON-ODOI KUNEEMEKA**
CHELSEA inajiandaa kumpa ofa ya mshahara mpya wa pauni 50,000 kwa wiki winga wake, Callum Hudson-Odoi (18), ikiwa ni ongezeko kubwa na litakaloifanya ofa nyingine kutoka Bayern Munich kukwama. ***(Mail)***

**DORTMUND YACHIMBA MKWARA**
MKURUGENZI wa soka wa Borussia Dortmund, Michael Zorc amezionya klabu zinazoshiriki Ligi Kuu England kuacha kumwania winga wa zamani wa Manchester City na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, 18. ***(Mirror)***

**HIGUAIN KUIVAA ARSENAL**
CHELSEA inajipanga kukamilisha haraka mchakato wa usajili wa straika wake mpya raia wa Argentina, Gonzalo Higuain (31) kutoka Juventus ili aweze kuitumikia katika mechi dhidi ya Arsenal itakayochezwa leo Jumamosi. ***(London Evening Standard)***

**PAREDES KITAELEWEKA EPL**
CHELSEA inakaribia kukamilisha mchakato kumsajili kiungo wa Zenit St Petersburg na Timu ya Taifa ya Argentina, Leandro Paredes (24) kwa dau la pauni milioni 31. ***(Express)***

**SPURS YAMGANDA MALCOM**
MABOSI wa Tottenham wamepeleka tena ofa katika klabu ya Barcelona ili kuwania saini ya mshambuliaji Mbrazili, Malcom ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Independent)***

**ARSENAL, JUVE VITANI**
ARSENAL inajipanga kumsajili mshambuliaji wa SC Braga na Timu ya Taifa ya Vijana ya Ureno (U-19), Francisco Trincao, baada ya kwenda kuvutiwa na nyota huyo ambaye pia anawaniwa na Juventus. (Tuttomercatoweb - in Italian)

**MCTOMINAY AWINDWA**
CELTIC itaendelea na mchakato wa kumwania kiungo wa Manchester United, McTominay lakini itawasilisha rasmi maombi ya kumsajili kama itapoteza kiungo katika kikosi chake hicho cha Parkhead. ***(Daily Record)***

**MADRID YAIPIKU UNITED**
BEKI wa Porto na Timu ya Taifa ya Brazil, Eder Militao (21) ambaye anatakiwa na Manchester United, tayari ameshafikia makubaliano ya kujiunga na Real Madrid. ***(SporTV via Mirror)***

**MCKENNIE ANUKIA LIVERPOOL**
LIVERPOOL iko katika mchakato wa kumwania kiungo wa Schalke na Timu ya Taifa ya Marekani, Weston McKennie ambaye sasa ana umri wa miaka 20. ***(Sun)***

**MINGS ANUKIA WEST HAM**
BEKI wa Bournemouth ambaye ni raia wa England, Tyrone Mings (25) anatakiwa kwa mkopo na klabu ya West Brom ambayo inashiriki Ligi Kuu England. ***(Sun)***

**RANIERI AMTAKA DABO**
KOCHA wa Fulham, Claudio Ranieri ameweka wazi nia yake ya kumsajili kiungo wa Fiorentina na Timu ya Taifa ya Burkina Faso, Bryan Dabo (26). ***(Sun)***

## HABARI MICHEZO

### Mwandembwa, Nsajigwa, Mwashiuya wafungiwa

Na Mwandishi Wetu

MWAMUZI Mashaka Mwandembwa amefungiwa kuchezesha soka kwa muda wa miezi mitatu kutokana na kushindwa kutafsiri vizuri sheria ya kuotea katika mechi iliyochezwa Novemba 3 mwaka huu kati ya JKT Tanzania dhidi ya Simba ambayo ilimalizika kwa mabingwa hao watetezi kupata ushindi wa mabao 2-0.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, ilisema kuwa adhabu hiyo aliyopewa Mwandembwa imetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 39 ya Ligi Kuu Toleo la 2018 kuhusu Udhibiti kwa Waamuzi.

Ndimbo alisema pia Kamati ya Saa 72 imetoa onyo kwa Mwamuzi Msaidizi, Mbaraka Rashid kwa kutokuwa makini wakati wa akichezesha mechi hiyo.

Alisema pia Kocha Msaidizi wa Singida United, Shadrack Nsajigwa amefungiwa mechi mbili na kupigwa faini ya Sh. 500,000 baada ya kuondolewa kwenye benchi la ufundi kwa kosa la kupinga maamuzi ya Mwamuzi huku Kocha wa Makipa wa African Lyon, Juma Bomba naye akifungiwa mechi mbili na kupigwa faini ya sh. 500,000 baada ya kuondolewa kwenye benchi la ufundi kwa kosa la kupinga maamuzi ya mwamuzi.

Ndimbo alisema pia Singida United imetozwa faini ya Sh. 200,000 kutokana na timu yake kutoingia kwenye chumba cha kubadilishia nguo badala yake kuingia kwenye chumba cha waandishi wa habari wakati Mbao na Alliance FC kila moja ikipigwa faini ya sh. 500,000 kwa kushindwa kuingiza timu za U-20 kwenye mechi ya utangulizi.

Naye Godfrey Mwashiuya wa Singida United amefungiwa mechi tatu na kupigwa faini ya Sh. 500,000 baada ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kosa la kumpiga mpinzani wake ngumi kwa makusudi wakati mpira ukiwa umesimama katika mechi dhidi ya Biashara United ambayo ilimalizika kwa suluhu.




Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira (kushoto), akionyesha nembo ya Mbio za Kilimanjaro Marathon ili kuashiria uzinduzi rasmi wa mbio hizo mwaka huu. Wengine ni wadau na wadhamini wa mbio zinazofanyika kwa mwaka wa 17 hapa nchini. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# ZAWADI KILI MARATHON KUWABEBA WATANZANIA

Na Godfrey Mushi, MOSHI

WANARIADHA wa Tanzania watakaofanikiwa kuibuka washindi katika nafasi ya kwanza na ya pili kwenye mbio za Kilimanjaro Marathon zitakazofanyika Machi 3 mwaka huu mjini hapa watapewa zawadi zaidi, mbali na zawadi za kawaida, imeelezwa.

Uamuzi huo umetangazwa ili kuongeza hamasa kwa wanariadha wa hapa nchini kujiandaa vyema na hatimaye kumaliza katika nafasi za juu kwenye mbio hizo.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Meneja Mauzo na Usambazaji wa Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Mwamba Stanslaus alisema kampuni yao inajivunia kudhamini mbio hizo kwa miaka 17 na kusema mshindi wa kwanza kwa upande wa wanaume na wanawake kwa mbio za kilomita 42 ataondoka na kitita cha Sh. milioni 20.

Mwamba alisema kuwa endapo wanariadha wa Tanzania watamaliza katika nafasi ya kwanza kwa wanaume na wanawake watapewa zawadi ya Sh. milioni 1.5 wakati wale wanataomaliza kwenye nafasi ya pili kila mmoja ataondoka na zawadi ya Sh. milioni moja moja.

Alisema mbio maarufu za kilomita 5 maarufu kama Fun Run, zinazodhaminiwa na Grand Malt pia zitafanyika ambapo zitashirikisha wanariadha wenye rika.

"Hizi ni mbio za kujifurahisha kwa hivyo watu wa rika zote wanakaribishwa kushiriki ili pia iwe kama sehemu ya mazoezi huku wakipata kinywaji chao cha Grand Malt chenye afya tele," alisema meneja huyo.

Naye Meneja wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Lilian Mwalongo alisema: "Tigo tunajivunia kuwa wadhamini wakuu wa mbio za Tigo Kili Half Marathon kwa mwaka wa nne mfululizo. Tukiongoza sokoni kwenye mageuzi ya maisha ya kidijitali."

Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira ambaye alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa mbio hizo aliwapongeza wadhamini na waandaaji kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye maandalizi ya mbio hizo.

"Hakika mmezifanya mbio hizi kuwa maarufu zaidi na pia mmeendelea kutangaza mkoa wa Kilimanjaro, nawashukuru sana. Nitoe wito kwa wafanyabiashara kutumia fursa hii vizuri kwani ndio muda muafaka wa kufanya biashara tofauti tofauti," alisisitiza kiongozi huyo.

Aliwataka wafanyabiashara wa Moshi hasa wenye hoteli za ngazi zote, kuanza kufikiria kutoa ofa mbalimbali ili washiriki watenge muda zaidi wa kukimbia lakini pia kufanya utalii mkoani humo.

# Kijangwani kusajili wachezaji watano

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya Kijangwani inayoshiriki Ligi Daraja la Pili Wilaya ya Mjini imesema inatarajia kusajili wachezaji wapya watano ili kuimarisha kikosi chake kuelekea mzunguko wa lala salama wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Hassan Juma alisema wanatarajia kusajili washambuliaji wawili, golikipa mmoja pamoja na mabeki wawili na wanaamini baada ya kupata nyota hao wapya, timu yao itafanya vizuri katika ligi hiyo yenye ushindani.

Juma alisema wachezaji hao ambao wanatarajia kuwasajili kutoka katika zilizoko mkoa wa Central kwa kuwaandalia mechi maalum za kirafiki ili kuwapima uwezo wao na endapo wataonyesha viwango vizuri watawasajili.

**"Kwenye usajili wetu, tutaangalia zaidi katika timu za Central ,tutakuwa na mechi za mazoezi za mara kwa mara ili kuwapima uwezo wao wachezaji ambao tutawasajili, hii itatusaidia kuangalia viwango vyao na mapungufu yao ili tujue tunasajili wachezaji wa aina gani," alisema Juma.**

Kijangwani ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Daraja la Pili Kundi A lenye timu 13 ikiwa na pointi 11.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Zanzibar (ZFA), Mohamed Ally "Teddy" amesema mwenendo wa usajili kwa vilabu vya Ligi Kuu Zanzibar unasuasua tofauti na timu zinazoshiriki madaraja mengine.

Teddy alizitaja timu tatu ambazo zimechukua fomu ili kufanya usajili mpaka jana kuwa ni pamoja na Malindi, Mlandege na vinara wa Ligi Kuu Zanzibar, KVZ.



Michezo

Jumamosi Januari 19, 2019

Nipashe



## Rashford kulipwa mshahara mnono

HABARI UK 30



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita itakayochezwa leo, jijini Kinshasa, DR-Congo. **PICHA : HISANI YA SSC**

# SIMBA, AS VITA HAPATOSHI LEO

●●●Kocha wa Wekundu wa Msimbazi asisitiza wamekwenda kusaka ushindi na si...

**Na Somoe Ng'itu**

INAWEZEKANA! Hii ndiyo kauli mbiu ya wawakilishi wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ambao wanatarajia kuwavaa wenyeji AS Vita leo kwenye Uwanja wa Martyrs mjini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Mechi hiyo ya Kundi D inatarajiwa kuchezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania, wakati mchezo mwingine wa kundi hilo ulikuwa ni kati ya JS Saoura ya Algeria dhidi Al Ahly ya Misri ambao ulifanyika jana usiku.

Simba ambayo ilikuwa haijashiriki hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa muda wa miaka 15 itashuka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-0 walioupata dhidi ya JS Saoura kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Simba Mbelgiji, Patrick Aussems, amesema mechi yao ya leo haitakuwa rahisi kutokana na timu zote mbili kuwa na rekodi nzuri msimu huu katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Aussems alisema kuwa Simba haijaenda Kinshasa kwa ajili ya kuzuia na badala yake wameenda kusaka ushindi ili kutimiza malengo yao ya kutinga hatua ya robo fainali. "Itakuwa mechi ngumu lakini hatujaja hapa kuzuia, tumekuja hapa kujaribu kutengeneza nafasi kama ilivyo kwa michezo yetu mingine na kujaribu kufunga."

Kiungo wa Simba, Haruna Niyonzima, alisema katika mkutano wa waandishi wa habari jana kuwa wanawaheshimu wapinzani wao lakini watahakikisha wanapata ushindi na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutinga hatua ya robo fainali.

"Kila mechi kwetu ni sawa na fainali, tumekuja kupambana ili kupata pointi tatu, tumejipanga kuonyesha uwezo wetu, hatujaja kutembea," alisema Mnyarwanda huyo ambaye anafahamu Kifaransa.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, aliliambia gazeti hili kuwa wanajua ushindani uliopo katika mechi zote za hatua ya makundi, lakini wanaamini timu yao ina nafasi ya kusonga mbele.

Kocha Mkuu wa AS Vita, Florent Ibenge amesema kuwa anaamini leo ataibuka na ushindi katika mechi ya leo na kufufua matumaini ya kusonga mbele.

"Tumepoteza mechi moja, ila zimebaki mechi tano, tunaamini tutafanya vizuri, tumeifuatilia Simba, tunaijua inavyocheza," alisema kocha huyo alipozungumza na King-fut.

Katika mechi ya leo, AS Vita itamkosa beki wake tegemeo, Dharles Kalonji ambaye alionyeshwa kadi nyekundu kwenye mechi ya kwanza ugenini dhidi ya Al Ahly wakati mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wao watashuka dimbani bila ya nahodha wao, John Bocco na Erasto Nyoni ambao ni majeruhi.

# Zahera asisitiza mabao mapema

**Na Faustine Feliciane, Shinyanga**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ya jijini Dar es Salaam wanatarajia kuwakabili wenyeji Stand United katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Kambarage mkoani hapa.

Yanga ilitua mkoani hapa tangu juzi tayari kwa mchezo huo bila la viungo wake wawili wa kimataifa, Papy Tshishimbi na Thabani Kamusoko ambao ni majeruhi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, alisema kuwa mechi zote za Ligi Kuu Bara ni ngumu zaidi kwao kwa sababu kila timu wanayocheza nayo inajiandaa kuvunja rekodi ya kutofungwa wanayoishikilia.

Zahera alisema amewaandaa wachezaji wake kupambana na kusaka mabao mapema ili kuongeza morali na kuifanya kazi ya kusaka pointi tatu kuwa nyepesi.

"Huwa nawaambia tuhakikishe tunamaliza mechi ndani ya dakika 30 za kwanza, hii itatupa nguvu na kumaliza kipindi cha pili vizuri, nafurahi hili wanaanza kulitekeleza," alisema kocha huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Yanga yenye pointi 53 ndio vinara wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >